

**KIKOI Vazi la kale lisilochuja utamu**

UKURASA 13




**Arsenal yapata kundi mchekea Europa Ligi**

UKURASA 22





# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Oktoba 4, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580358

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## RIPOTI MAALUMU

# Wasiojulikana watafuna mamilioni ya Muhimbili

UKURASA 4



Mgombea Urais kupitia CCM, Dk. John Magufuli pamoja na Mgombea Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya chama hicho, Dk. Hussein Mwinyi na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na viongozi wengine wa CCM wakicheza wimbo wa hamasa wa "Tanzania ya Sasa, ya Magufuli", wakati wa mkutano wa kampeni katika viwanja vya Mnazi Mmoja, mjini Unguja jana. **PICHA: IKULU**

# Kamati ya Maadili NEC yamwonya Tundu Lissu

UKURASA 2

# Magufuli aanika mikopo mahususi kwa Zanzibar

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# Mama Samia afunda vijana vurugu kampeni za uchaguzi

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA Mwenza wa urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan, amewataka vijana kutokubali kushawishiwa kujiingiza katika vurugu ili uchaguzi uingie dosari na mataifa ya nje yaingilie.

Alitoa rai hiyo jana wakati akizungumza na wananchi wa mjini Igunga mkoani Tabora katika mfululizo wa ziara yake ya kampeni.

"Vijana wetu wanakuja kushawishiwa kwa njia mbalimbali, toweni taarifa kwamba kuna jambo linapikwa na linanukia," alisema.

Alisema wananchi lazima watambue kuwa lengo linalotafutwa hapa ni uchaguzi uingie dosari na mataifa ya nje yaingilie, ili ionekane Tanzania haitawaliki na mambo ya kuleta maendeleo yawe yanakwenda polepole.

"'Speed' tunayokwenda nayo ya maendeleo inawatisha wengi na wengine hawafurahishwi mambo yanavyokwenda nchini, tusikubali, msichokozeke, msipandikizwe vurugu ndani ya maendeleo," alisema.

Mama Samia alisema wanaochochea vurugu na kuvunjika kwa amani na utulivu kimsingi wameshanusa harufu ya kushindwa vibaya na hivyo wanachokifanya ni kuchochea vurugu zitokee nchini.

"Msikubali vurugu zitokee maeneo yetu, vurugu hazichagui uwapo kwenye mpango wa vurugu na asiyekuwapo, likilipuka limelipuka," alisema.

Mama Samia alisema katika kipindi cha miaka mitano ijayo, serikali imejipanga kwenda kwa kasi zaidi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za maji, afya, elimu, umeme, kilimo na miundombinu.

Makamu wa Rais huyo pia aliwaomba wananchi wajitokeze kwa wingi siku ya Oktoba 28, mwaka huu kuwapigia kura rais, wabunge na madiwani wa CCM ili serikali iendelee kuwaletea maendeleo.

Alisema kunapokuwa na mchanganyiko wa madiwani, Baraza la Madiwani wa Halmashauri linakuwa linatumia muda mwingi kulumbana kwenye vikao na hivyo kuzorotesha maendeleo.

# JPM aanika mabilioni yaliyokopwa mahususi kwa miradi ya Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, ameweka hadharani kiwango cha fedha kilichokopwa na Serikali ya Tanzania kwa lengo la kugharamia miradi ya maendeleo visiwani Zanzibar katika miaka 40 iliyopita.

Amesema kuwa katika kipindi hicho cha miongo minne, Sh. trilioni 2.3 zilikopwa na serikali mahususi kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo visiwani hapa, hivyo wanaosema muungano hauna faida kwa Zanzibar ni waongo.

Dk. Magufuli alibainisha hayo wakati akinadi sera zake na kuomba kura kwa wananchi maelfu waliokuwa wamefurika kwenye Viwanja vya Mnazimmoja visiwani hapa kumsikiliza.

Alisema muungano huo una faida kubwa, ukiwezesha kuwa na taifa moja lenye mshikamano mkubwa na wa kutolewa mfano wa kuigwa barani Afrika.

"Ukimsikia mtu anasema muungano hauna faida, ujue ana upungufu wa kitu kichwani. Dk. Magufuli alisema.

Aliahidi kuwa endapo akichaguliwa tena kuongoza nchi, atamaliza kero za muungano zilizobaki kama alivyofanya katika deni la Sh. bilioni 22.9 la umeme ambalo Zanzibar ilikuwa inadaiwa na Shirika la Umeme (TANESCO).

Dk. Magufuli pia alimsifia Dk. Shein kwa maendeleo aliyoyafanya katika kipindi chake cha uongozi kwa miaka mitano iliyopita, akisema amefanikiwa kukuza uchumi wa Zanzibar hasa kupitia sekta ya utalii, kilimo, uimarishaji wa miundombinu ya barabara na kujenga soko la kisasa. Vilevile, alisema mgombea urais wa Zanzibar (CCM), Dk. Hussein ni mtu mvumilivu na mchapakazi, akikumbusha utendaji wake katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa muda wa miaka 15.

"Dk. Mwinyi ni mwaminifu, mchapakazi na mwadilifu na ndiyo nilipokuwa Rais, sikuona mtu mwingine wa kumpa Wizara ya Ulinzi na ndiyo maana nikampa yeye," alisifu.

Aliwaomba Wazanzibar kumchagua Dk. Mwinyi, akiahidi kushirikiana naye kwa maslahi ya Zanzibar hasa kwenye sekta ya mafuta na gesi ambayo alisema inapaswa kuwa na faida kwa Zanzibar.

"Ukitaka utamu wa sukari uonje, mpeni kura Dk. Mwinyi Wazanzibari awe Rais wenu, ana uwezo mkubwa wa kutunza amani," Dk. Magufuli alisema.

Mwenyekiti huyo wa CCM alitaka Dk. Mwinyi kuhakikisha anateua Makamu wa Pili wa Rais kutoka Kisiwani Pemba ikiwa atashinda nafasi hiyo ili kuondoa mgawanyiko kati ya Pemba na Unguja.



Mgombea Mwenza wa Kiti cha Urais kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akikabidhi Kitabu cha Ilani ya CCM ya 2020/25 kwa Mbunge Mteule wa Jimbo la Nzega Vijijini, Hamis Kigwangala aliposimama kwa ajili ya kusalimiana na wanachama wa chama hicho na wananchi wa Jimbo la Nzega Vijijini, akiwa njiani kuelekea Wilayani Nzega, mkoani Tabora kuendelea na mikutano wa kampeni jana. **PICHA: OMR**

# NEC yamwonya Tundu Lissu

**Na Enock Charles**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kupitia Kamati ya Maadili, imemwonya mgombea wa urais (CHADEMA), Tundu Lissu, kuhusu msimamo wake wa kuendelea na kampeni licha ya kuzuiwa.

Juzi, Kamati ya Maadili ilitangaza kuzuia kampeni kumzuia mgombea huyo kuendelea na kampeni zake kwa siku saba baada ya kutuhumiwa kukiuka kanuni za maadili ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Hata hivyo, muda mfupi baada ya kutangazwa kwa zuio hilo dhidi yake, Lissu aliitisha kikao na waandishi wa habari nyumbani kwake jijini Dar es Salaam na kusisitiza kuwa anakusudia kuendelea na kampeni zake kutokana na kile alichokiita tume kutumika kumhujumu.

Wakati Lissu akitangaza dhamira yake hiyo, Kamati ya Maadili jana ilimtaka kutekeleza adhabu iliyompa, ikionya kuwa kuendelea na kampeni kutamgharimu zaidi.

Katibu wa Kamati hiyo, Emmanuel Kawishe, alisema kama ti yao ilikuwa sahihi kupeleka kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA barua ya wito wake kwa Lissu kwa kuwa ndiye mdhamini wa mgombea urais kupitia chama hicho tofauti na inavyodaiwa na Lissu kuwa alitakiwa kupewa barua yeye mwenyewe.

"Tume inawasiliana na Katibu Mkuu na siyo vinginevyo, hivyo madai ya Bwana Lissu kwamba hajapokea barua ya malalamiko mpaka leo ni uongo, chama chake kilipokea barua na malalamiko yaliwafikia yakimtaja kwa jina lake yeye mwenyewe.

"Adhabu inatakiwa kutekelezwa kwa kuwa imetolewa na chombo chenye mamlaka ya kisheria na kwa kuzingatia taratibu, mgombea urais kupitia CHADEMA anatakiwa kuheshimu na kutekeleza adhabu hiyo kama ilivyotolewa," Kawishe alisema.

Alifafanua kuwa katika kipindi chote cha siku saba za adhabu hiyo zilizoanza jana, Lissu haruhusiwi kujinadi na hata kuwapigia kampeni wagombea wengine wa nafasi za ubunge na udiwani, lakini wagombea wa nafasi hizo wanaruhusiwa kumnadi.

HABARI KITAIFA

# Safari treni Arusha-Dar kuongezwa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

SHIRIKA la Reli (TRC), limesema liko tayari kuongeza safari kutoka nne kwa wiki kutoka Mkoa wa Arusha mpaka jijini Dar es Salaam kulingana na idadi ya abiria itakavyoongezeka.

Vilevile, TRC imepunguza bei ya usafiri huo kutoka Sh. 18,000 hadi Sh. 16,000 ili kusaidia wananchi wanyonge kutumia usafiri huo.

Mwenyekiti wa Bodi ya TRC, Prof. John Kandoro alibainisha kuwapo kwa mpango huo jijini Arusha wakati wa mapokezi ya treni ya abiria kwa mara ya kwanza iliyowasili mkoani humo kutoka jijini Da es Salaam baada ya miaka 30 kupita bila kuwapo usafiri huo.

Alisema pia wapo mbioni kuanzisha usafiri wa treni kutoka Arusha hadi Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Hii ni kutokana na upendo wa serikali kwa wananchi wake kutaka kusaidia usafiri rahisi na hasa kipindi hiki tunachokwenda cha uhitaji mkubwa wa usafiri," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenan Kihongosi, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Idd Kimanta, alisema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 15 kukarabati miundombinu ya reli, ili kurejesha usafiri wa treni.

Alisema Rais John Magufuli anahitaji kupongezwa kutokana na uzalendo wake huo na kupitia uboreshaji wa miundombinu na ununuzi wa ndege uliowezesha ongezeko la watalii na kupandisha uchumi wa nchi.

"Ninaomba mpongeze serikali, msisikilize wahuni wachache wanaomtukana Rais wetu kwa kupinga yote aliyofanya, kosa la Rais Magufuli lipi wakati ametufanyia mengi ambayo hatuwezi kuyasema hapa?" alihoji.

"Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, haki hiyo anapewa nani kama siyo Magufuli? Ninaomba vijana wenzangu mpeni haki na kumwombea na kumuunga mkono rais wetu.

"Ninaomba msisikilize watu wanaohamasisha kufanya vurugu na serikali haichezewi, hatuwezi kuruhusu watu 1,000 wachezee amani ya watu milioni moja, anayehamasisha vurugu, kitakachompata atasimulia na ukoo wake, siwezi kukubali mama yangu apigwe au mzee wangu apigwe, sitakubali lazima tulinde amani ya nchi yetu," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa nchini (TAKUKURU), Brigedia Jenerali, John Mbungo akikata utepe kufungua jengo jipya la taasisi hiyo, wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# DAS abaini kiini mauaji wazee

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Shinyanga, Boniphace Chambi, amesema uchunguzi walioufanya kuhusu mauaji dhidi ya wazee, umebaini familia na ndugu wa karibu ndiyo wahusika wakuu wa kadhia hiyo.

Kiongozi huyo alisema mjini hapa juzi kuwa familia pamoja na ndugu wa karibu, wamekuwa wakiwatuhumu wazee hasa wenye macho mekundu kuwa ni wachawi na kufikia hatua ya kupanga njama ya kuwatoa uhai kwa kuwakata kwa mapanga.

Chambi alikuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani, akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, katika Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga yalikofanyika kiwilaya.

Alisema jamii inapaswa kubadilisha mitazamo yao potofu na kuwatunza wazee ambao wao ni baraka na siyo kuwatuhumu kwa uchawi na kuwaua kikatili.

"Tunashukuru Mungu kwa sasa mauaji ya wazee yatokanayo na imani potofu za kishirikina yamepungua tofauti na miaka ya nyuma ambapo hali ilikuwa mbaya sana," alisema Chambi.

Katibu wa Baraza la Wazee wilayani huko, Boniphace Boaz, akisoma risala, aliishukuru serikali kupunguza tatizo hilo la mauaji dhidi ya wazee na kuomba elimu iendelee kutolewa.

Vilevile, Boaz ambaye pia ni daktari mstaafu, alisema kuna haja vyombo vya dola kuendelea kuwakamata waganga wa jadi wanaopiga ramli chonganishi, akisisitiza kuwa ni chanzo kingine kikuu cha mauaji na ukatili dhidi ya wazee.

Kiongozi huyo wa baraza pia aliishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa kuwapatia kadi za matibabu bure wazee 5,568, huku zingine 7,859 zikiendelea kutengenezwa. Alibainisha kuwa kwa sasa halmashauri hiyo ina jumla ya wazee 13,176.

Mratibu wa Shirika la Kutetea Haki za Wazee (Tawale) mkoani Shinyanga, Eliasenya Nnko, alisema kuwa kwa kushirikiana na serikali, wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kuwathamini wazee na kuwatunza.

Alisema kazi hiyo inafanyika sambamba na kukemea matukio ya ukatili dhidi ya kundi hilo na kuwezesha huduma za matibabu kwa wazee bila malipo.

# Waziri aipongeza SGA ukuzaji wa teknolojia

**Na Mwandishi Wetu,**
GEITA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), ameipongeza Kampuni ya SGA Tanzania kwa kukuza teknolojia baada ya kuibuka mshindi wa tatu wa jumla kwenye maonyesho ya kimataifa ya teknolojia ya madini yaliyofanyika mjini Geita.

Angela Kairuki, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye maonyesho hayo, aliipongeza kampuni hiyo inayojishughulisha na utoaji wa huduma kwenye sekta ya ulinzi, kwa kuingiza teknolojia za kisasa hasa kwenye sekta ya madini.

Maonyesho hayo yalishirikisha washiriki mbalimbali kutoka Tanzania na nje ya nchi.

Waziri Kairuki alisema SGA Tanzania imesaidia kutoa elimu kuhusu teknolojia za kisasa zinazosaidia kwenye utoaji wa huduma za ulinzi nchini.

Meneja wa Mauzo na Masoko wa SGA Tanzania, Faustine Shoo, alisema tuzo hiyo ni ishara kuthibitisha ubora za huduma zinazotolewa hasa kwenye uwekezaji wa teknolojia uliofanywa na kampuni hiyo katika kipindi chote tangu kuanzishwa kwake.

"Tumethibitisha namna teknolojia mpya za ulinzi zinaweza kusaidia kuboresha ulinzi kwenye maeneo ya migodi na kupunguza uwezekano wa kupata hasara.

"Kwa teknolojia hizi, migodi ya madini itakuwa sehemu salama kwa ajili ya kufanya kazi na serikali itafikia kusidio lake la kudhibiti bidhaa za madini kwaa ajili ya maendeleo ya uchumi," alisifu.

Meneja huyo alisema SGA Tanzania inafanya kazi na kampuni kubwa za madini nchini na faida zake zimeonekana kwa kuwa migodi mingi imedhibiti shughuli zake na kuimarisha ulinzi.

Mkurugenzi wa SGA Tanzania, Eric Sambu, alisema amefurahishwa na kutambuliwa kwa kampuni yake katika utoaji wa huduma bora, akitamba kuwa imethibitisha kwamba wanaweza.

Aliwapongeza wafanyakazi wa kampuni hiyo kwa kuonyesha uwezo mkubwa katika masuala ya ukuzaji wa teknolojia na kutoa huduma zinazoakisi thamani ya fedha za wateja.

Alisema ulinzi ni suala muhimu kwenye uwekezaji katika sekta ya madini kwa kuwa inaongeza tija na SGA Tanzania inajivunia kwa kushiriki kutimiza hayo. "SGA Tanzania ni kampuni ya kwanza binafsi kutoa huduma za ulinzi hapa Tanzania na imeonyesha umahiri wake kutokana na kuwa na timu yenye motisha.

"Kwa timu ya wafanyakazi 18,000 kwenye kampuni iliyoanzishwa miaka 50 iliyopita, dhima na dira yetu ni watu. Tumewekeza zaidi kwenye mafunzo na tunahakikisha kwamba tunalipa zaidi ya viwango vya soko kuwapa motisha na kuhakikisha hawahami," alisema.

Alisema wakati kampuni inaadhimisha miaka 36 ya uwepo wake nchini, kumekuwapo na ukuaji hasa kipindi cha miaka mitano iliyopita kutokana na mapinduzi na shughuli ambazo zimekidhi matarajio ya wateja.


**KUPOTELEWA NA "CERTIFICATE OF INCENTIVE**

**KAMPUNI YA GOLDSTAR PAINTS TANZANIA LIMITED,** INAYO JIHUSISHA NA UTENGENEZAJI RANGI TANZANIA BARA. INATANGAZA KUPOTELEWA NA **"CERTIFICATE OF INCENTIVE No 041197,** ILIYOTOLEWA NA TANZANIA INVESTMENT CENTER (T. I. C) TAREHE 08/01/2007. KWA YEYOTE ATAKAE IONA ANAOMBWA KUIWAISILISHA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI / OFISI YA GOLDSTAR PAINTS TANZANIA LIMITED AU OFISI ZA TANZANIA INVESTMENT CENTER (T.I.C) AU AWASILIANE NASI KUPITIA NO **+255 759 003 979/+255 655 007 939.** Taarifa ya polisi: **DAR/KIL/RB/708350/2020**



**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO. 53/2020**

**WILFRED JULIUS KASAMBALA:::::::::::::::::: MDAI**

**DHIDI YA**

**JOYCE EZEKIEL KASHILILIKA::::::::DAIWA WA KWANZA**

**NMB BANK PLC:::::::::::::::::::::::::MDAIWA WA PILI**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: JOYCE EZEKIEL KASHILILIKA**

Fahamu kwamba mdai amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 05/10/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. T. Munzerere Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu. Byaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anaeruhusiwa kisheria. Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya Mjini.

**Kumbuka:** Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 07/09/2020.

RIPOTI MAALUM

# Wasiojulikana watafuna mamilioni ya Muhimbili




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Dk. Respicious Boniface.

**Na Mary Geofrey**

KAMUSI ya Kiswahili Sanifu Toleo la Mwaka 2004 inatoa tafsiri ya neno 'mgonjwa' kuwa ni mtu aliye na maradhi au maumivu fulani katika mwili wake.

Katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), wagonjwa wamegawanywa katika makundi mawili ambayo ya wagonjwa wa kawaida na wagonjwa mahututi wanaohitaji uangalizi maalumu wa wataalamu wa afya.

Vilevile, kwenye kundi la pili lenye wagonjwa mahututi, kuna wagonjwa ambao wanafikishwa hospitalini huko kupatiwa matibabu wakiwa hawatambuliki kwa majina wala maeneo wanakoishi.

Wataalamu wa afya katika taasisi hiyo wamelibatiza kundi hilo la wateja wao kwa jina la 'wagonjwa wasiotambulika'. Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, anasema wagonjwa hao ni wanaopata ajali barabarani na kusaidiwa na wasamaria wema na wale wanaookotwa maeneo mbalimbali nchini wakiwa wamepoteza kumbukumbu.

Dk. Respicious Boniface, katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salam, anabainisha kuwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, taasisi hiyo imetumia Sh. milioni 80.8 kutoa matibabu kwa wagonjwa wasiotambulika.

Anafafanua kuwa kwa mwaka 2017 pekee, walipokea wagonjwa 46 wa kundi hilo, saba wakitibiwa katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) na 39 wodi za kawaida. Kati yao, wanne walipoteza maisha.

Dk. Boniface anasema kwa mwaka huo, walitumia Sh. milioni 24.76 kuwatibu wagonjwa hao, zikijumuisha Sh. milioni 2.7 zilizotumika kwa ajili ya chakula na Sh. 8.4 za upasuaji.

"Kwa kipindi hicho cha mwaka 2017 katika gharama hizo za matibabu, Sh. milioni 1.8 zilitumika kwa ajili ya wagonjwa wa ICU, Sh. milioni tano kwa waliolazwa wodi za kawaida na Sh. milioni 9. 2 zilitumika kwa ajili ya ushauri, uchunguzi na dawa za kulevya, hivyo jumla kuwa Sh. milioni 24.76 zilizolipwa na MOI," anafafanua.

Kwa mwaka 2018, Dk. Boniface anasema walitumia Sh. milioni 18.2 kwa ajili ya kuwatibu na kuwapa mahitaji muhimu wagonjwa wasiotambulika 32. Kati yao, watano walilazwa ICU, 27 wodi za kawaida. Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa mmoja alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu.

Anasema kuwa Sh. milioni 18.2 zilizotumika mwaka huo kulihudumia kundi hilo zilijumuisha gharama za ICU Sh. milioni 1.7, wodi za kawaida Sh. milioni 4.5, ushauri, uchunguzi na dawa za kulevya Sh. milioni 6.4, chakula Sh. milioni 1.9 na upasuaji Sh. milioni 5.4.

Kwa mwaka uliofuata (2019), mkurugenzi huyo anabainisha kuwa walipokea wagonjwa wasiotambulika 44. Kati yao, watano waliwekwa ICU na 39 walitibiwa katika wodi za kawaida, huku wawili wakifariki dunia wakiwa hospitalini huko.

Anabainisha kuwa wagonjwa hao 44 waliigharimu taasisi hiyo Sh. milioni 27 zikijumusiha Sh. milioni 2.1 za huduma za ICU, Sh. milioni 8.1 kwa wodi za kawaida, Sh. 264,000 za chakula, Sh. milioni 8.8 kwa ajili ya ushauri, uchunguzi na dawa za kulevya pamoja na Sh. milioni 7.8 zilizotumika katika upasuaji.

Dk. Boniface anabainisha kuwa, katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu, walipokea wagonjwa wasiotambulika 19. Kati yao, wawili waliwekwa ICU, 17 wodi za kawaida. Anasema wagonjwa 18 walipona na mmoja alipoteza maisha.

Anaendelea kufafanua kuwa, katika miezi hiyo sita, taasisi hiyo ilitumia Sh. milioni 10.6 kuokoa maisha ya wagonjwa hao, zikiwamo Sh. 560,000 zilizotumika kugharamia huduma za ICU, Sh. 238,000 kwa wagonjwa wa kawaida, Sh. milioni 3.8 kwa ajili ya ushauri, uchunguzi na dawa za kulevya, Sh. 114,000 za chakula na Sh. milioni 3.8 za malipo ya upasuaji.

Mkurugenzi huyo anasema MOI imekua ikipokea majeruhi wa ajali kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine na inatumia gharama hizo kuwatibu na kuwatunza.

Anasema kundi hilo la wagonjwa wasiotambulika linafikishwa hospitalini huko na wasamaria wema na vyombo vya dola, hasa Jeshi la Polisi.

"Mnapokea majeruhi lakini ni 'unknown' (wasiofahamika), mtu anapata ajali, anaumia sehemu ya kichwa au sehemu nyingine ya mwili, anapoteza fahamu na kufikishwa hospitali akiwa hana kumbukumbu, inabidi taasisi itumie fedha zake kumtibu," anasema.

Dk. Boniface anafafanua kuwa, kwa kuwa MOI ni hospitali ya umma na jukumu lake msingi ni kuokoa maisha kabla ya mambo mengine, kundi hilo la wagonjwa hupatiwa matibabu stahiki na mgonjwa anapozinduka na kurejesha kumbukumbu, taratibu zingine huwa zinafuata ikiwamo kuwatafuta ndugu zake.

Hata hivyo, anasema baadhi ya wagonjwa hao hushindikana kuwapata ndugu zao kutokana na kupata majeraha makubwa na hivyo kushindwa kurejesha kumbukumbu zao hata baada ya kukamilika kwa matibabu.

"Katika hili, huwa tunalazimika kutafuta utaratibu wa kuwatafuta ndugu kwa kuwatangaza kwa kutumia picha zao na ndugu wanapoona, hujitokeza na kuwachukua wapendwa wao," anasema.

Anaongeza kuwa taasisi hiyo kupitia Kitengo cha Ustawi wa Jamii, imekuwa ikiwasafirisha baadhi ya wagonjwa wasio na ndugu au waliotelekezwa na kuwafikisha kwenye vijiji vyao katika mikoa mbalimbali nchini.

Dk. Boniface anaanika kikwazo kingine kwamba licha ya kuwatangaza, baadhi ya wagonjwa huwa hawapati ndugu zao, hivyo kulazimika 'kuishi' hospitalini kwa muda mrefu, akibainisha kuwa kuna waliowahi kukaa hospitalini huko hadi miaka mitatu wakiigharimu taasisi mamilioni ya Sh. kuwahudumia.

**NDUGU KUTOROKA**

Meneja Ustawi wa Jamii na Uhusiano wa MOI, Juma Almas, anasema MOI hutumia sehemu ya mapato yake kulitibu na kulihudumia kwa chakula kundi hilo la wagonjwa.

Almas anadokeza kuwapo kwa tatizo la baadhi ya ndugu wa wagonjwa kuchukua uamuzi wa kutoroka baada ya kuwaona ndugu zao wakiwa katika hali mbaya hospitalini huko.

"Kuna ndugu wanajitokeza wanamwona mgonjwa wao ndani ya wiki moja hadi mbili. Wakipewa gharama za matibabu au wakiambiwa kuna kipimo au dawa za kununua, wanaondoka na hawarudi tena," anasema.

Meneja huyo anabainisha kuwa tatizo hilo lina ushuhuda mkubwa kwa wagonjwa waliovunjika uti wa mgongo, walioumia kichwani na waliopooza.

"Maisha ya watu wengi wa mjini ni ya kubangaiza, hivyo unapopata tatizo kubwa namna hiyo ndugu wakija siku mbili tatu, unawaambia 'kanunue dawa fulani', anapotea siku tatu humuoni. Sasa, hospitali inabaki na dhana kuwa huyu mgonjwa ana ndugu kumbe washaingia mitini," anasema.

Almas anaendelea: "Ndugu wa aina hiyo wanawaathiri wagonjwa kisaikolojia kwa sababu wagonjwa hawahitaji tu kulipiwa gharama za matibabu, bali faraja kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki."

Anasema baadhi ya wagonjwa wanaookotwa na wasamaria wema, hufikishwa hospitalini huko wakiwa na vitambulisho, lakini wengi wao hufika wakiwa wameibiwa kila kitu, hivyo kuwa na ugumu katika kuwapata ndugu zao.

"Wengi wao ni wagonjwa wanaofikishwa hospitalini baada ya kupata ajali za barabarani kama watembea kwa miguu, waendesha baiskeli na pikipiki na wachache ni mareruhi walioanguka kwenye majengo marefu au wagema minazi," anabainisha.

Almas anashauri ndugu wa wagonjwa kutoogopa kujitokeza kuwajulia hali ndugu zao na kuzungumza na hospitali ili kufahamu cha kufanya badala ya kujificha.

"Elimu inahitajika zaidi kwa jamii, ndugu anapopata ajali ajitokeze ili wafanye mazungumzo na hospitalini kuangalia namna ya kuokoa maisha ya mgonjwa wao," anashauri.

■ITAENDELEA WIKI IJAYO

## Majaliwa ataja sifa za rais wa kupewa kura

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania watakaopiga kura Oktoba 28, mwaka huu, kumpa kura mgombea atakayewaunganisha ili waendelee kuwa wamoja na atakayetumia rasilimali za nchi kwa manufaa ya wote.

Alisema katika uchaguzi ujao, wananchi wanatakiwa kutulia na kuchagua kiongozi bora anayeshirikisha watu katika maendeleo yao na kuwaunganisha kuwa kitu kimoja.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akimwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli, katika mkutano wa kampeni uliofanyika kwenye viwanja vya Magufuli mjini Kahama.

Alisema Watanzania watakaompa kura Dk. Magufuli katika uchaguzi wa mwaka huu, watakuwa wamefanya uamuzi sahihi kwa kuwa anaweza kusimamia na kuratibu rasilimali za wananchi kwa kiwango cha juu.

Majaliwa ambaye pia ni Waziri Mkuu, alisema kuwa kuelekea uchaguzi huo, Watanzania wanatakiwa kulinda tunu ya amani ya nchi kwa kuwa imekuwapo tangu zamani, nchi ilipopata uhuru.

Aliwataka wananchi kuwabeza watu wanaopitapita na kutukana na kuongeza kuwa, kiongozi mzuri ni yule anayelinda utawala wake pamoja na majeshi ya nchi.

Mgombea ubunge wa Bukombe mkoani Geita (CCM), Dotto Biteko, alisema Wilaya ya Kahama ni moja ya maeneo ambayo yanakusanya mapato yake yatokanayo na madini.

# Mbaroni tuhuma kwa kuua mpenzi, mtoto

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi mkoani Mara, linamshikilia mkazi wa Sengerema mkoani Mwanza, Fredrick John (20), kwa tuhuma za kuua watu wawili akiwamo mpenzi wake, Doris Samson.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Daniel Shillah, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa, John pia anatuhumiwa kumuua mtoto Nicson Charles (5) ambaye ni mdogo wa Doris.

Kamanda Shillah alisema mauaji hayo yalitokea Septemba 25, mwaka huu wilayani Bunda mkoani Mara, chanzo kikidaiwa wivu wa mapenzi.

"Fredrick alikuwa anaishi na kufanya shughuli zake Sengerema na Doris alikuwa anaishi Bunda. Siku ya tukio, Fredrick alikwenda kumtembelea mpenzi wake na ndipo walipogombana baada ya Doris kutaka waondoke wote na mwenzake kutoafiki," alisema.

Kamanda Shillah alisema wawili hao waligombana na ndipo John aliposababisha kifo cha mpenzi wake.

Aliendelea kueleza kuwa kutokana na mtoto Nicson kushuhudia mauaji hayo, mtuhumiwa huyo aliamua kumnyonga.

"Baada ya mauaji hayo, Fredrick alizificha maiti kila moja iliwekwa kwenye kochi lake kwenye sebule na kuwafungia mlango," alisema.

Kiongozi huyo wa polisi alisema kuwa baada ya mauaji hayo, mtuhumiwa aliiba simu ya marehemu Doris pamoja na luninga yake na kukimbilia Mwanza.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Jumatano, mtaa wa Ilemela mkoani Mwanza na alipohojiwa, alikiri kufanya mauaji hayo ya mtu na mdogo wake.

Kamanda alisema mtuhumiwa huyo katika mahojiano, pia alikiri kuiba vitu nyumbani kwa mpenzi wake huyo ambavyo kwa sasa wanavishikilia kwa ajili ya ushahidi.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Wilaya ya Muheza, Al-Shaymaa Kwegyir (kushoto), akiwa na mgombea ubunge Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' (wa pili kushoto) na mgombea udiwani Kata ya Mtindiro, Mustafa Hatibu (kulia) wakijiburudisha kwa kinywaji cha alkasusi, katika eneo la msikiti mkuu wa Ijumaa, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wizi wa maandishi tatizo kwa taaluma

**Na Vincent Mpepo,** OUT

PROFESA Mugyabuso Mulokozi, amesema wizi wa maandishi ni tatizo linalorudisha nyuma maendeleo katika sekta ya elimu hususani katika maandalizi ya wataalamu wenye weledi kwenye taaluma.

Mtumishi huyo wa zamani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), aliyasema hayo juzi wakati wa warsha ya uandishi wa kitaaluma inayofanyika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Aliwaeleza washiriki madhara yatokanayo na vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kupata wahitimu wasiokidhi vigezo na ubora wa soko katika sekta ya umma na binafsi.

Profesa Mulokozi alibainisha mbinu mbalimbali za kutambua wizi wa maandishi katika matini, machapisho na tasnifu ikiwa ni pamoja na kuangalia kurasa za mwanzo za tasnifu zikilinganishwa na kurasa za ndani.

"Kutokana na ukweli kuwa Watanzania wengi siyo mahiri wa Kiingereza, mara nyingi kurasa za mwanzo za tasnifu huandikwa na mwanafunzi mwenyewe, kitu kinachoweza kumsaidia mhadhiri kugundua wizi wa maandishi kirahisi akifananisha na kurasa za ndani kwa kuangalia aina ya lugha katika sehemu hizo," alibainisha.

Profesa Mulokozi alisema katika kudhibiti wizi wa maandishi, watahini wa ndani na wa nje wanapaswa kutekeleza kikamilifu kazi yao ili kupata kazi bora za kitaaluma.

Alisema pamoja na uwapo wa teknolojia zinazosaidia katika ugunduzi wa wizi wa maandishi, bado kuna tatizo la tasnifu zinazofanyika kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa lugha hiyo haijangizwa kwenye mifumo hiyo ya kiditali.

Washiriki katika warsha hiyo walijadili mbinu mbalimbali za wizi wa kitaaluma, wakieleza kuwa kadhia hiyo inatokana na uvivu, uzembe na uhitaji wa kuhitimu kwa sababu za kupanda madaraja.

Mhadhiri Newton Kyando wa OUT alisema pamoja na vikwazo vingine, lugha ya kufundishia ndiyo kiini cha tatizo la wizi wa maandishi ya kitaaluma katika taasisi nyingi za elimu ya juu.

"Wapo wanafunzi ambao wanafanya wizi wa maandishi ya kitaaluma kwa sababu za kutoelewa lugha zinazotumika kufundishia katika kuelezea dhana fulani, hivyo kujikuta wameingia kwenye wizi," alisema.

Alisema kwa uzoefu wake amekutana na mazingira ya wanafunzi ambao wanatetea hoja kwa lugha ya Kiswahili, lakini hawawezi kuelezea kwa Kiingereza, hivyo kulazimika kuchukua maandiko ya Kiingereza ili kujazia pangapopungua kukidhi maelezo ya dhana husika.

Mkuu wa Kitivo cha Sheria, Dk. Rindstone Ezekiel, alisema mwendelezo wa wizi wa maandishi unatokana na majukumu mengi walionayo wahadhiri, hivyo kukosa muda wa kupitia kazi hizo kwa umakini.

"Changamoto nyingine inatokana na uwapo wa wanataaluma ambao wanaridhika kwa kuangalia tu kazi kwa juujuu na mwonekano wa nje," alisema Dk. Ezekiel.

Aliongeza kuwa katika taasisi nyingi za elimu ya juu, wapo watu ambao wanafanya shughuli za kusaidia wanafunzi kuandika utafiti na tasnifu na mara nyingi ofisi zao ziko maeneo jirani na vyuo.

Mhadhiri Msaidizi kutoka UDSM, Zamda Geuza, alisema matatizo mengi ya wizi wa maandishi ya kitaaluma yatadhibitiwa ikiwa wadau wote wataheshimu maadili ya kazi na wajibu wao katika nafasi zao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watu wanaorubuni wapigakura wachukuliwe hatua za kisheria

**TANGU** kuanza kwa kampeni kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani uliopangwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, kumekuwa na ripoti kuhusu matukio mbalimbali yanayokinzana na kanuni na sheria za uchaguzi kama ilivyoainishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Siku hadi siku kwenye vyombo vya habari kumeripotiwa taarifa za watu kufanya vurugu kwenye mikutano ya uchaguzi, matusi na kejeli dhidi ya wagombea wa upande mwingine na hata kuchanwa kwa picha na mabango ya baadhi ya wagombea.

Lakini kama hayo hayatoshi, katika baadhi ya maeneo, kumekuwapo na taarifa kwamba kuna makundi ya watu yanapita kwa wapigakura na kuwalaghai ili kuwapa vitambulisho ya kupigia kura kwa madai kwamba wanafanya hivyo kwa lengo la kuwapatia mikopo kutoka taasisi za kifedha.

Miongoni mwa maeneo hayo ni mkoani Dodoma ambako imedaiwa kuwa watu hao wamekuwa wakipita na kuwarubuni watu kwa kisingizio hicho.

Madai hayo yaliibuliwa hivi karibuni na uongozi wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Dodoma kwamba kuna watu wameanza kupita na kuchukua vitambulisho hivyo wakiahidi kuwapatia mikopo, jambo ambalo si kweli kwa kuwa wamekuwa wakichukua na kwenda kutengeneza nakala inayofanana na kitambulisho hicho.

Hatua hiyo ni ukiukwaji mkubwa wa sheria ya uchaguzi na kwamba inawanyima fursa wapigakura kwa kuwa itawafanya washindwe kutimiza haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua kiongozi wanayempenda.

Kwa kufanya hivyo, wananchi hao, kwa maneno mengine wanauza uhuru wao kwani watu hao wanaopita kukusanya vitambulisho hivyo, wanafanya hivyo kwa manufaa yao ya kisiasa.

Jambo hilo si mara ya kwanza kufanyika kwani kabla ya vitambulisho vya kupigia kura, kulikuwa na shahada ambazo watu wa aina hiyo walikuwa wakizinunua kwa urahisi huku wamiliki ama wakipewa fedha kidogo au kurubuniwa kwa madai ya kwenda kuzihakiki.

Kwa kiasi kikubwa, mtindo huo ulikuwa ukifanywa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa kwa kuwarubuni au kuwanunua wafuasi wa upande mwingine wa kisiasa kwa lengo la kudhoofisha wapinzani wao. Hilo pia lilikuwa likifanyika katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa yakionekana kuwa na nguvu ya chama fulani cha siasa.


Aidha hata sasa jambo hilo linafanyika kwa malengo kama ya zamani ya kudhoofishana kisiasa lakini wananchi hao wanaokubali kutoa vitambulisho hivyo, si kwamba wanakosa fursa ya kupiga kura bali pia kupoteza nyaraka muhimu kwa mahitaji mbalimbali.

Pia ifahamike kwamba watu wanaofanya hivyo, kwa kuchukua kadi za kupigia kura, wanakiuka sheria za nchi kwa mujibu wa kifungu cha 90(2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343, ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kuchukua ya kadi ya mpigakura iliyotolewa kwa mtu mwingine.

Kwa kuwa jambo hilo linaweza kutia doa katika uchaguzi, ni vyema vyombo vya dola vikachukua hatua kwa kuwafuatilia watu wanaoendekeza tabia hiyo na kuwachukulia hatua za kisheria.

Mamlaka husika pia, ikiwamo Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ni vyema zikatoa tamko na elimu kwa wananchi ili watambue kuwa kuuza au kununua kadi ya mpigakura ni kosa la jinai.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Stendi ya mabasi ya mikoani Mbezi isikose huduma hii

Na Sabato Kasika

**MABASI** ya mikoani ambayo yamekuwa yakitumia stendi ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, yatarajia kuhamishiwa Mbezi Mwisho wiki chache zijazo ili kuendelea kutoa huduma huko.

Kuhamia kwa mabasi hayo Mbezi Mwisho, kunatokana na maelekezo ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Joseph Nyamhanga.

Nyamhanga alitoa maagizo hayo kwa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Spora Liana, kuhakikisha mabasi yaendayo mikoani yanahamia katika stendi hiyo inayojengwa eneo la Mbezi Mwisho.

Katibu huyo anataka mabasi hayo yahamishiwe stendi mpya ya Mbezi kabla ya Oktoba 15 na kuacha stendi ya Ubungo kwa kuwa ni mali ya mradi wa mabasi yaendayo haraka. Ujenzi wa stendi ya mabasi yaendayo mikoani na nchi za jirani, unaoigharimu serikali Sh. bilioni 50.9, unaelezwa na Liana kuwa umefikia hatua nzuri ya kukamilika.

Inalezwa kuwa stendi hiyo itakakuwa na uwezo wa kuchukua mabasi zaidi ya 700 kwa wakati mmoja, ikiwa ni ongezeko la zaidi ya mabasi 400 ambayo yamekuwa wakitumia stendi ya Ubungo.

Aidha, stendi hiyo mpya inatajwa kuwa ni ya kipekee katika ukanda wa Afrika Mashariki na kati, na kwamba itakuwa ni suluhisho la kukosekana kwa stendi bora jijini Dar es Salaam.

Baada ya kueleza kwa kifupi kile kinachoendelea katika stendi hiyo na sifa zake, sasa ninataka nijikite zaidi kwenye suala la huduma za zimamoto, kwamba ni muhimu ziwapo katika stendi hiyo.

> **Baada ya kueleza kwa kifupi kile kinachoendelea katika stendi hiyo na sifa zake, sasa ninataka nijikite zaidi kwenye suala la huduma za zimamoto, kwamba ni muhimu ziwapo katika stendi hiyo.**

Kwa kuwa ni stendi ya kipekee katika ukanda wa Afrika Mashariki na kati, ni vyema kila huduma zikapatikana hapo na hasa ya zima moto ambayo itasaidia kuepusha majanga ya moto yanayoweza kujitokeza.

Ni ukweli usiopingika kwamba, stendi ya Ubungo haina huduma nyingi ikiwamo hiyo ya zimamoto, ambayo ni ya muhimu, hivyo hali hiyo isijirudie kwenye stendi ya kisasa inayojengwa Mbezi Mwisho.

Kama stendi ina uwezo wa kuchukua mabasi 700 halafu haina huduma ya zimamoto, hilo litakuwa ni tatizo, kwa kuwa basi moja likipata hitilafu na kuwaka moto zinaweza kuteketeza mengine.

Lakini huduma hiyo ikiwapo, itakuwa rahisi kuzima moto unaowaka, lakini kama itakuwa ni kusbiri huduma hiyo kutoka eneo la Fire, itakuwa ni hatari, hasa kutokana na jiji kujaa foleni za magari.

Hivyo, wakati jijini la Dar es Salaam likiendelea kusimamia ujenzi huo, lihakikishe kwamba huduma ya zimamoto ni miongoni mwa zile muhimu zitakazopatikana katika stendi hiyo ya kisasa.

Yawezekana stendi hiyo ikawa na zahanati, sehemu ya kulala wageni, migahawa, vyoo na nyingine nyingi za muhimu, lakini kuwapo wa huduma ya zimamoto ni muhimu kwa usalama wa abiria na vyombo vya usafiri.

Ninatambua kuwa uwekezaji huo wa stendi, utasaidia kuboresha huduma za usafiri nchini na kuongeza uwekezaji kupitia biashara kwa kuwapo maeneo yaliyotengwa kwa watoa huduma na wafanyabiashara wa ngazi zote.

Wote hao wanahitaji usalama, hivyo bado kuna umuhimu mkubwa wa kuwapo kwa huduma ya zimamoto ili kwamba, linapotokea janga la moto iwe rahisi kukabiliana nalo haraka na tena kwa wakati.

Pamoja na hilo, wapigadebe wasiruhusiwe kusogelea stendi hiyo, badala yake wawepo wahudumu wa mabasi husika watakaosaidia kuwaelekeza wageni kupata huduma mbalimbali zikiwamo za usafiri.

Kuruhusu wapigadebe itakuwa ni sawa na kruhusu vitendo vya wizi na unyanyasaji wa abiria kama ambavyo imekuwa ikifanyika kwenye stendi ya Ubungo ambayo sasa itahamia Mbezi Mwisho.

Stendi hiyo mpya inatajwa kama ya kipekee, hivyo upekee huo usiruhusu kuwapo kwa vitendo vyovyote viovu kwa abiria na watu wengine, hivyo wapigadebe waishie ubungo.

Ninasema hivyo kwa sababu wanawadhalilisha abiria kwa kuwavuta huku na kule na wakati mwingine kuwaibia mizigo, wanapowagombania kila mmoja akitaka ampeleke katika basi analotaka bila ridhaa ya abiria.

# SAFU

## FIKRA MBADALA

# Hawa nao kweli waheshimiwa?



Nkwazi Mhango, Canada

HUWA napata utata na wakati mwingine kinyaa itajwapo heshima sijui cheo cha mheshimiwa! Hushangaa sana hasa nionapo baadhi ya wanaoitwa waheshimiwa. Wengine hawana wala hawastahili heshima. Wananuka ubabaishaji, ufisadi, urongo na uzushi. Ni mafisadi na mafisi hadi kwenye mifupa. Mfano, wanaotembeza uongo mchana wakati huu wa kusikia mengi wanaoendelea kuitwa waheshimiwa.

Hivi kweli hawa ni waheshimiwa? Wana heshima gani iwapo wanatenda mambo ya aibu wazi? Wanaotetea wezi wa rasilimali zetu nao eti ni waheshimiwa! Makuwadi wa uchukuaji wanaoita uwekezaji au vibaraka wa mabeberu ambao Rais John Magufuli amekuwa akipambana nao, kweli nao ni waheshimiwa? Wapo wengi wake kwa waume.

Ukiwaona wana sura za binadamu. Lakini ndani ni mafisi watupu.

Je, sisi tunaowaita hawa waishiwa waheshimiwawakati tunajua ni majizi tunastahiki heshima kweli? Je, heshima ni maneno au matendo? Sheria inasema: Mhalifu ni yule aliyetenda kosa la jinai au aliyeshuhudia asiripoti au aliyeshirikiana na aliyelitenda; ni yeyote anayeshiriki kutenda kosa la jinai ima kwa kujua au kutojua hadi atakapobainika vinginevyo. Je, hawa wanaotafuta madaraka kwa rafu ni waheshimiwa kweli? Hebu angalia yafuatayo:

Kwanza, kwa maneno na matendo yao, hawastahili heshima; unapomdharau mtu usitegemee akuheshimu wala ukimdanganya mtu usitegemee akutetee.

Pili, ukiangalia historia zao za utendaji na mazingira hata sera na nia zao, hutahofia wala kusita kuwaita wabangaizaji na wasaka tonge tena wa kukodiwa au kununuliwa.

Tunao wengi. Wapo majukwaani, vyamani na kwingineko. Tunao kwa mamia hawa. Wengine wanatafuta madaraka kujitajirisha huku umma ukiendelea kusota. Ukiwaona utawajua.

Hupenda kujisifu na kulaumu tu bila kutoa mbadala. Sasa mnawajua; msiseme hatukuonya Ibilisi wa mtu ni mtu. Aweza kuwa wewe hata mimi.

Aweza kuwa mtukufu hata tajiri na msomi. Ibilisi ni ibilisi hata aitwe mchungaji, mheshimiwa, kizito na mfadhili na makando kando mengine mengi.

Tatu, anayetetea ujinga utakaoweza kutufanya Watanzania kulanguliwa umeme siyo jizi tena kubwa lao? Na huyu aliyesababisha madini yetu kuwaneemesha wawekezaji ilhali sisi tunazidi kuwa maskini si wa kuogopwa kama ukoma? Vipi kuhusiana na mtu asiye na sera za kutukomboa bali kututumia badala ya kututumikia; anayetaka kuwe watwana naye bwana? Hebu fikiria juu ya mtu anayetoa toa ahadi asitekeleze hata moja. Waswahili husema: Haja ya mja kunena, muungwana vitendo. Je asiyetimiza hili si muongo tu hata akiitwa mheshimiwa?

Nne, mfikirie anayewadanganya watu. Anasema hili leo kesho lile. Je huyu anayostahiki hata chembe kuitwa mheshimiwa? Mbona uheshimiwa umevamiwa kiasi cha kuwa

uishiwa? Mbona uheshimiwa umekosa thamani kiasi cha kutumiwa na wazushi hata wambea?

Tano, kuna watu na heshima zao. Lakini pia wapo wengi waitwao waheshimiwa wasiostahili hata nusu ya heshima. Wapo wenye silka, hulka na tabia za wanyama waitwao waheshimiwa. Kuna watu wanapaswa kuwa gerezani si bungeni wala uraiani.

Chukulia, mpotoshaji wa wazi wazi akilenga kuchonganisha watu. Fikiri jitu au mijitu inayoeneza chuki za kidini na kikabila.

Sita firiki zaidi. Hebu jielekeze kwa mtu anayesimama kwenye viwanja kama vile vya Jangwani akatangaza kutenda miujiza iwe ya kisiasa au ya kidini wakati hana lolote bali janja ya kuwaibia wajinga wengi.

Je hawa hawapo? Siku moja tulikuwa tunajadili ni kwanini nchi za kiafrika haziendelei ilhali zimekuwa na serikali kwa zaidi ya miaka 50. Tuligundua mdudu mmoja mbaya sana akiziangamiza nchi hizi. Anaitwa ulafi na ubabaishaji na kutegemea miujiza badala ya kuchapa kazi.

Tembelea Afrika kuanzia Kaskazi hadi Kusi, Mashariki na Magharibi. Utakuta watu wanaojifanya wanawapenda watawaliwa waliwa. Watajionyesha kama wapenda maendeleo wakati ni vikwazo vya hayo maendeleo ndoto. Wanaishi maisha ya kifalme wakizungukwa na makapuku wa kunuka.

Wao na familia zao, kupitia ujambazi fichi wa kimfumo hawana tofauti na kupe. Wanawanyonya watu maskini kwa kisingizio cha upuuzi uitwao kuchaguliwa!

Wanaficha mabilioni ya fedha Ulaya. Wanachekiwa afya zao na kutibiwa Ulaya.

Leo akitokea rais asiyeruhusu uhuni huu anaambiwa anaogopa kwenda nje! Kwani kuzurura ni kazi ya rais? Wameua hospitali, zahanati, shule, mashamba, viwanda na kila aina ya mradi.

Halafu akitokea mtu akavifufua wanampa kila aina ya majina. Bado majizi hawa wanawahadaa watu wanaweza kuwaletea maendeleo. Kwao watu ni familia na marafiki zao.

Wameishiwa kiasi cha kushindwa hata kujitambua. Bahati mbaya na watawaliwa nao wameendelea kuuziwa mbuzi kwenye gunia kana kwamba

hawana akili wala macho!

Hata nifungwe au kupigwa mijeledi, sitawaheshimu waheshimwa majambazi waliotamalaki kwenye nchi za kiafrika. Sitaacha kuwaambia kuwa ni majizi na waishiwa.

**Leo sisemi sana.**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Wenye ulemavu wamesahaulika kampeni!



Na Joseph Kulangwa

KAMPENI za uchaguzi mkuu zinaendelea nchini kote. Wagombea na vyama vyao wanazunguka nchi nzima kwa njia za barabara, anga na maji, kuwafikia wapiga kura ili kuomba ridhaa ya kuchaguliwa.

Ushawishi ni mkubwa kila mahali, ili mradi kila mtu siku ya mwisho avune anachokipanda leo, na kushuhudiwa atakayecheka na atakayelia. Hata hivyo mambo yanakwenda kwa amani na utulivu mkubwa, kama ilivyo ada ya Watanzania.

Ni vizuri kuendelea kuvipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kusimama kidete na kujipanga, kuhakikisha kuwa ni amani kwanza, ndiyo itatuvusha katika kinyang'anyiro hiki. Ni vizuri kwamba wananchi wanaendelea kutoa ushirikiano kwa vyombo vyao.

Watanzania wanapata fursa ya kufika kwenye mikutano ya kampeni na wale wanaoangalia mbashara kwenye vyombo vya habari kama luninga na kusikiliza kwenye redio na kusoma magazeti, kuna wanachopata na kukifanyia kazi.

Wapiga kura wanaotazamiwa kujitokeza Oktoba 28 kupiga kura, wana kazi kubwa ya kuchekecha na kuona ni upi mchele na zipi ni chuya. Kauli ni tamutamu kutoka kwa wagombea, takrima nazo hazikosi hapa na pale ingawa kimyakimya. Unyenyekevu ni mkubwa pia.

Jambo la msingi ni kuamua nani atafaa kuwa rais, nani afaa kuwa mbunge na nani atastahili kuwa diwani. Hilo ni chaguo la mpiga kura na ni siri yake na sanduku la kura, kwa kuwa ndiye mshawishika na ndiye mwamuzi.

Kinachofanywa na wagombea na wapambe wao, ni kutafuta jinsi ya kushawishi na kupata kura zitakazowatosha kupewa ridhaa hiyo adhimu, hivyo ni vizuri kumakinika katika hilo na kuchagua mtu stahiki kabisa.

Mpiga kura atakayefanya kosa katika kuchagua amtakaye, atajutia kwa miaka mingine mitano ijayo. Ni dhahiri wapo waliokosea mwaka 2015 na sasa wataamua kuwa makini wasirudi walikotoka.

Ndiyo sababu wagombea na wapambe wao wana nafasi finyu sana katika uchaguzi, kwa sababu mwamuzi ni mpiga kura mwenyewe, kwa kuzingatia kile anachoamini kwa mgombea anayemtaka.

Tumeshuhudia utamu wa maneno ili kuvutia kura, lakini pia vitisho dhidi ya mpiga kura kuchagua mtu ambaye mpambe hamtaki kwa maslahi yake. Lakini kwa kuwa kura ni siri, halitaharibika jambo, kwa sababu hatuchagui sura wala wajihi bali uwezo wa mtu.

Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alipata kusema, kwamba hatuchagui kabila kwa sababu hatutambiki na kama tunachagua sura ni vyema mpiga kura akanywe chai na mgombea wake mwenye sura nzuri. Kinachochaguliwa ni sifa na uwezo wa kuwakilisha.

Pamoja na yote haya, ni dhahiri kwamba kampeni zinazofanywa zimegubikwa na ubaguzi. Si wa rangi, si wa wajihi, si wa sura wala wa kabila, dini au ufupi, urefu, wembamba na unene, la hasha, bali wa kasoro za kimaumbile.

Tunao watu wenye ulemavu mbalimbali ambao kwa ulemavu wao, hawawezi kufuatilia kampeni kwenye mikutano ya hadhara, televisheni, redio wala magazeti, lakini wana haki ya kuchagua na hata kuchaguliwa.

Mathalan, wenye ulemavu wa kusikia na kuona. Wameandaliwa mazingira gani ya kufuatilia kampeni? Ni lini imeshuhudiwa mkutano wa kampeni wakiwapo wakalimani waliosimama mbele na wagombea wanaojinadi na wao kutafsiri?

Ziko wapi ilani za uchaguzi zilizoandikwa kwa nuktanundu kwa ajili ya wenzetu wasioona? Yote haya bila shaka yanajulikana, lakini ni dhahiri hayakufanyiwa maandalizi mapema, na matokeo yake haki hiyo inapotea na wenzetu hawa wenye ulemavu wanabaki kuangalia tu na wasifanye lolote.

Haki yao ya msingi kidemokrasia inapotea hivi hivi, kana kwamba si washiriki wa ujenzi wa demokrasia ndani ya nchi yao huru.

Tunapongeza kuwa tumetumia fedha zetu za ndani takriban Sh bilioni 300 na ushei kuendesha uchaguzi, iweje zinufaishe walio timamu tu? Haki iwe kwa kila Mtanzania bila kujali upungufu wake kimaumbile.

## KONA YA UKWELI



Na Thobias Mwanakatwe

# Wagombea wanaposhindwa kutii makubaliano kanuni za uchaguzi

INAFAHAMIKA kuwa dhumuni la kila chama cha siasa kinapoanzishwa ni kutaka kushika dola Au kwa maneno mengine kuingia Ikulu.

Kwa utaratibu wa Tanzania, uchaguzi wa Rais, wabunge, Madiwani na Wawakilishi hufanyika kila baada ya miaka mitano. Oktoba 28, mwaka huu, uchaguzi huo utafanyika kwa ajili ya kupata Uwakilishi huo.

Kabla ya kufikia siku ya uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imekuwa ikifanya maandalizi ya uchaguzi kwa kuendesha semina na makongamano ya viongozi na wanachama wa vyama vya siasa. Lengo la kufanya hivyo ni kuwawezesha wazifahamu kanuni na sheria za uchaguzi.

Baada ya kupewa elimu hiyo, NEC imejiwekea utaratibu ambapo vyama vinavyoshiriki uchaguzi hutia saini makubaliano ya kutekeleza kanuni za uchaguzi ambazo lengo lake ni kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

Uwapo wa kanuni za uchaguzi ni msingi ambao huviwezesha vyama vya siasa kufanya kampeni zao kwa kwa mujibu wa sheria za nchi ikiwamo Sheria ya Tume ya Uchaguzi.

Utaratibu wa kutia saini makubaliano hayo ni msingi ambao unapozingatiwa na vyama na wagombea huepusha malalamiko yanayoweza kuathiri shughuli za kisiasa na kusaidia nchi inapata viongozi sahihi pamoja na kulinda amani na utulivu wa nchi.

Tangu kampeni zimeanza Agosti 16, mwaka huu, swali ambalo Watanzania wengi wanajiuliza ni je, wagombea na vyama vyao wanatekeleza sheria na kanuni za uchaguzi kama ambavyo walitia saini makubaliano?

Hili ni swali ambalo kila mtu anapaswa kutafakari na kulitafutia majibu kwa wakati wake na kuja na majibu au ufumbuzi wa tatizo hilo iwapo majibu yake yataonyesha kuwa sheria na kanuni hazifuatwi.

Binafsi, naona kwamba katika kipindi hiki cha kampeni wapo baadhi ya wagombea ambao hawazingatii kanuni na sheria za uchaguzi na kujiona kama vile wao wapo juu ya sheria.

Ukichunguza kwa undani utabaini kuwa wanaozikiuka kanuni za uchaguzi ni hao hao ambao wamekuwa wakijipambanua katika vyama vyao kwamba ni magwiji kama si wabobezi wa sheria za nchi.

Inatia mashaka kwa sisi ambao tunategemea wagombea hao wangetuongoza na kutufundisha umuhimu wa utii wa sheria bila shurti lakini cha ajabu wao ndio kwanza wanakuwa vinara wa kuzikiuka sheria hizo.

Najiuliza kama walikubali tena bila kulazimishwa wala kushikiwa mtutu wa bunduki kusaini makubaliano ya kanuni za uchaguzi iweje leo hii watu hao hao wawe ndio wa kwanza kuzikiuka.

Viongozi wa namna hii wanawezaje kuwa na ujasiri wa kushawishi wananchi wawapigie kura, inatia ukakasi.

Lakini kibaya zaidi viongozi hao wanapobainika kukiuka maadili ya kanuni za uchaguzi wanapoitwa wakajieleze kwenye taasisi zinazosimamia uchaguzi wanakataa na kutoa maneno ya kejeli kwa viongozi wa taasisi husika.

Napata shaka kama kweli viongozi hao kabla ya kuingia kwenye kinyang'anyiro walipata muda mrefu wa kutafakari hizo nafasi wanazoziomba ni kweli wataweza kuzitendea haki.

Nilimpenda kiongozi mmoja mstaafu akiwa kwenye kampeni mkoani Manyara, aliwaambia wananchi wasifanye makosa katika kuchagua Rais kwa sababu suala la kuongoza nchi si sawa na kucheza kamali.

Wengi wanaweza wakawa hawakumuelewa kiongozi huyo alikuwa anamaanisha nini, lakini ukweli ni kwamba wapo baadhi ya wagombea hawaonyeshi umakini katika kuomba nafasi wanazotaka wananchi wawachague.

Nasema hivyo kwa sababu haiwezekani wewe unaomba nafasi ya urais halafu bado unakuwa kinara wa kukiuka kanuni za uchaguzi ambazo wewe mwenyewe au chama chako kilizisaini na kukubaliana nazo.

Watanzania wenzangu kampeni zinazoendelea hivi sasa hapa nchini nadhani zimetupa somo na kuwafahamu aina ya wagombea na vyama vyao ambao nawaona kama ni watu wasiopenda amani iliyopo hapa nchini.

Wagombea wetu tumebakiza zaidi ya siku 20 kabla ya kuingia siku ya uchaguzi, nina imani bado mna nafasi ya kurekebisha tabia zenu kwa kuacha kuhubiri shari.

Watanzania hatujazoea vurugu tunapenda amani kwa hiyo chonde chonde mtambue kuna maisha baada ya uchaguzi, zingatieni kanuni za uchaguzi mlizozisaini wenyewe.

NEC msiwe wanyonge katika hili, mnapoona kuna mgombea au chama wanakiuka kanuni za uchaguzi shusheni rungu ili kulinda uchaguzi huu uwe na heshima.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU UBARIKI UCHAGUZI MKUU 2020**

**Kwa maoni na ushauri tuwasiliane; mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

# Uwazi na ukweli ni chachu katika kujenga ndoa imara

NDOA ni muunganiko wa watu wawili waliolelewa katika familia tofauti ambao kimsingi wamekubaliana kwa hiari yao kuishi pamoja na kushirikiana katika mambo mbalimbali yakiwamo ya furaha na huzuni.

Wawili hao wanaweza kutofautiana kuhusu namna ya kusimamia familia na kuhusu matumizi ya fedha. Wanaweza kutofautiana kuhusu fedha wanazopata kutokana na ajira au biashara.

Hata hivyo, kunapokosekana uwazi na uaminifu kuhusu fedha zao, hasa pale zinapopatikana, zinapopungua au kukosekana katika utunzaji wa familia, huweza kusababisha ugomvi na shida katika uhusiano.

Usiri katika mambo ya fedha au mali huhatarisha uhai wa ndoa, hivyo ni jambo muhimu na la msingi kwa wanandoa kuelewana juu ya mapato na matumizi ya fedha pamoja na malengo ya kiuchumi ya muda mrefu na muda mfupi.

Uwazi na maisha yenye mshikamano ni jambo la msingi kwa wanandoa. Kwa mantiki hiyo, wanandoa wanapaswa kutengeneza mazingira ya uwazi na ukweli katika maisha yao.

Mambo ya usiri juu ya fedha na mali imekuwa chanzo cha maumivu na migogoro katika ndoa nyingi, hasa pale mke au mume anapogundua kuwa alifichwa kuhusu jambo fulani. Mfano, imetokea mahali pengine kwamba, mke au mume anaweza kununua kiwanja, kununua gari, kujenga au kununua nyumba, kukopa fedha benki, kusaidia ndugu kifedha au kuanzisha mradi fulani bila mwenzi wake kujua.

Aidha, kumekuwa na usiri mkubwa miongoni mwa wanandoa juu ya vipato vyao. Limekuwa jambo la kawaida wanawake wengi kutokujua vipato vya waume zao.

Hali hii imekuwa msumari wa moto au mwiba mchungu katika mioyo ya baadhi ya wanandoa, hivyo, kuondoa tumaini na kusababisha wanandoa kutokuaminiana. Pendo la ndoa linadumaa kisha mapenzi yanakauka. Kila mmoja anapoteza hisia na mvuto kwa mwenzake.

Ndoa inabaki kuwa kama boksi la zawadi lililofungwa vizuri kwa nje na kupambwa, lakini ndani yake hakuna kitu. Kumbuka, kupoteza hisia ni kupoteza uhai wa ndoa.

Ni muhimu na busara kwamba wanandoa wazingatie sera ya uwazi juu ya kile wanachokipata na wanachotaka kufanya. Wafikirie athari zinazoweza kutokea kutokana na uamuzi ya kuwa wasiri na waongo kuhusu vipato vyao na matumizi yake ndani ya ndoa.

Kama kuna hali ambayo ni kikwazo kwa mke au mume inayopelekea kutokutaka kuwa muwazi kwa mwenzake, yafaa wanandoa kujenga tabia ya kupenda mazungumzo kwa lengo la kusaidiana, kurekebisha hali iliyopo na kuleta uponyaji katika ndoa.

Kutembea na machungu moyoni huathiri afya ya akili na mwili hata kusababisha kifo. Inashauriwa kwamba wanandoa watengeneze muda wa pamoja ili kupata nafasi ya kujadiliana kwa upendo na upole, kushauriana, na kushirikishana hisia zao, kwani mazungumzo hujenga boma zuri.

Ni muhimu ikafahamika kuwa, kuweka vinyongo moyoni hushawishi visasi. Na kwa kweli, roho ya visasi huwa haileti suluhu, bali huongeza maumivu na kuondoa uwepo wa Mungu. Roho ya visasi siyo njia nzuri ya kutatua tatizo.

Katika ndoa hakuna usiri baina ya mume na mke. Kila jambo katika ndoa nila wote. Kuwe na makubaliano kuhusu mambo ya msingi ya kufanya katika maisha ya ndoa. Uwazi katika kupangilia vizuri masuala ya fedha kutawezesha kujenga ndoa imara. Ndoa ni kitovu cha malezi na ustawi wa jamii na taifa. Kwa hiyo, ili kuwa na taifa lenye ustawi na maendeleo ni muhimu ndoa kuwa imara na zenye furaha.

Ndoa imara huongeza uhai wa ndoa na maisha ya wanandoa. Ndoa imara husababisha familia imara. Familia imara husababisha jamii imara na jamii imara husababisha taifa imara.

Kwa mantiki hiyo, ni muhimu wanandoa wakaelezana bayana juu ya vipato vyao, mali zao na jinsi watakavyovitumia kwa manufaa yao, watoto walio nao au wanaowatarajia na misaada watakayoitoa kwa watu mbalimbali.

Kila mmoja atambue nafasi yake na wajibu wake katika ndoa. Mke na mume wanapotambua nafasi zao na kutekeleza majukumu yao ipasavyo, hii huchochea maendeleo, amani, umoja, mshikamano, na mahaba katika ndoa. Kutoshirikiana na kutowajibika katika ndoa, husababisha manung'uniko, mvuto wa ndoa kupotea, hivyo, mpasuko katika ndoa hutokea.

Wanandoa wanapaswa kuwa na nia moja katika kuwaza, kupanga na kutenda. Uwepo wa mipango ya pamoja iliyotanguliwa na uwazi ni chanzo cha ustawi wa kiroho, kiuchumi na kifamilia ndani ya ndoa.

Fedha au mali walizozipata kutoka kwa wazazi wao wakati wa kuagwa, harusi au ndani ya ndoa zitakuwa zao pamoja na watoto wao badala ya mwenzi mmoja kuona ni zake na kwamba ndiye mwenye nguvu ya kiuchumi ndani ya ndoa.

Wanandoa wasisahau walikotoka pamoja katika maisha yao. Fedha na mafanikio visiondoe utu, thamani, na nafasi ya mke au mume ndani ya ndoa. Mpende zaidi mwenzi wako kuliko fedha, utabarikiwa katika kazi zako zote na uzao wako utakuwa heri.

■**Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare) inayojihusisha na masuala ya Ndoa na Malezi ya Watoto. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz**

# MAISHA

OKTOBA 4, 2020

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




HARUSI

Ukurasa 12



Ukubali utoto wanaofanya watoto

Ukurasa 10



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Pendezesha nyumba kwa gharama nafuu



Kashata za nazi

Ukurasa 14



## NYWELE BANDIA

## Raha na karaha zake

Ukurasa 14

# Ukubali utoto wanaofanya watoto

Na Moses Ismail

FIKIRIA kwa akili yako ya kiutu uzima, kwamba inawezekana kweli kukubali kumegewa 'aisikrimu' na rafiki zako kwa kutumia meno zake na kisha akakupa ili nawe uile?

Ni dhahiri jibu lake itakuwa haiwezekani. Ule mate zake? Si ndio mwanzo wa kuambukizana ugonjwa huo?

Achilia mbali 'aisikrimu' za kukatiwa na meno, hata kipande cha muhogo tu wa shilingi mia alioushikashika kwa mikono yake pia huwezi kukubalia akumegee na kuula.

Unajua kwa nini huwezi kufanya mambo hayo mawili? Kwa sababu wewe ni mtu mzima mwenye akili yako na unazejua madhara yatokanazo na maradhi mengi za kuambukiza kwa njia mikono na mate.

Rudi kwa watoto sasa, utakuta kundi la watoto hata sita, wanatoka shuleni au wanacheza tu mtaani, mmoja akinunua 'aisikrimu' au muhogo, ujue kundi zima watagawana kitu hicho bila kujali aliyenunua atawamegee kwa mikono michafu au kwa kuuma kwa meno yake.

Itokee sasa mzazi amekuta mwanae katika hali hizo, ya kumegewa kitu kwa njia hizo, lazima atawaka na kumfokea mwanae akimkataza kuacha ujinga huo kabisa. Utamsikia akifoka: "Hivi wewe hushibi? Si umekunywa chai nyumbani wewe? Halafu si nilikupa hela za kutumia"

Utafoka kwa sababu utaona kinachofanywa na mtoto wako na wenzake ni kama akili mbovu. Watagawiana vipi vitu vyakula kwa njia hizo?



Ni kweli, unampa fedha za kutosha kujinunulia mihogo na aisikrimu akiwa shule au mtaani, bila kutegemea wenzake. Ila bado anapenda kula mihogo na aisikrimu za kuchangia, anaakili mbovu?

"Hapana, si akili mbovu, nitabia ya kimaumbile ya wanyama." Anasema Simon Maende, mtaalamu wa saikolojia ya watoto.

Maende anafafanua: "Kwa kawaida wanyama, tukiwemo binadamu, tunatabia ya kula chakula kwa pamoja, kiwe kidogo au kingi. Ni tabia yetu ya asili, hata majumbani tunakula chakula kwa kuzunguka sinia au sahani moja."

"Hili linajenga ushirikiano, linaondoa ubinafis na choyo. Ila tunapo jitenga na tabia hii, tunapojenga ubinafsi na uchoyo na chuki zote kitu ambacho siyo tabia za asili za binadamu ila zinatengenezwa na hali ya maisha."

Maende anasema kisaikolojia jambo hili ni zuri na hujenga afya ya akili zao na linachochea upendo ingawa pia anakiri kuwa katika mazigira ya afya ni hatari pia.

"Kiafya ni tatizo," anasema: "Ila halipaswi kukemewa kwa nguvu, inabidi tu wazazi na walimu wawaeleweshe watoto madhara hayo ya kiafya kwa upole na kuwaelekeza namna nzuri ya kugawana vitu vya kula."

## NA KHAMIS KIDAGO 0657 207168 — QUIZ

**MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA**

**Le quiz du week – end**

1. Weka sentensi zifuatazo katika wingi.

**Mfano:** Une course incroyable – Des courses incroyables.

**a.** Un résultat très décevant
Des resultants très décevants

**b.** Un relais victorieux
Des relais victorieux

**c.** Une championne olympique
Des championnes olympiques

**d.** Un record battu
Des records battus

**e.** Un prix exceptionnel
Des prix exceptionnels

**f.** Un saut extraordinaire
Des sauts extraordinaires

**g.** Un titre précieux
Des titres précieux

**h.** Un prix special
Des prix speciaux

**i.** Une récompense méritée
Des récomponses méritées

**j.** Un château feodal
Des châteaux feodaux

**k.** Un bureau central
Des bureaux centraux

**l.** Un point capital
Des points capitaux

**m.** Un geste amical
Des gestes amicaux

**n.** Un détail spécial
Des détails spéciaux

**o.** Un test final
Des tests finaux

**p.** Un travail original
Des travaux originaux

**q.** Un vent glacial
Des vents glaciaux

**r.** Un scénario banal
Des scénarios banals

**s.** Un festival international
Des festivaux internationaux

**2.** Malizia sentensi zifuatazo kwa kuweka article le, la, l' au les.

- De quelle couleur est le drapeau(m) français?
- Comment s'appelle le (m)président de la (f)République française?
- Qu'est – ce que l'Élysée(m)?
- Quelle est la date de la (f)Fête nationale?
- À quelle fête sont associés les (m)œufs en chocolat?
- Qu'est – ce – que l'impressionisme(m)?
- Où se trouve l'embouchure(f) de la Seine (f)?
- Quelles sont les (f)cinq plus grandes villes françaises?
- À quel département correspond le (m)code postal 75006?
- Quelle est la (f)vitesse maximum du TGV?

**Le quiz du week – end**

**1. Bainisha kama maneno yafuatayo ni Masculin au Féminin.**

**Mfano:** Ballon rond – Masculin.


- Définition précise –
- Chanson espagnole –
- Don généreux –
- Leçon intéressante –
- Liaison incorrect –
- Feuilleton mensuel –
- Action particulière –
- Crayon noir –
- Façon élégante –
- Maison ancienne –
- Inscription definitive –
- Rayon lumineux –
- Son aigu –
- Wagon plein –
- Caleçon léger –
- Habitation curieuse –
- Balcon fleuri –
- Saison froide -
- Savon doux –
- Joli visage –
- Petit message –

## WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA



A lichokifanya daktari

WATOTO wengine bwana! Jamaa mmoja alikuwa na sh. 1000, alimtuma mtoto wa jirani akamnunulie maandazi ili anywe chai. Baada ya muda alimuona mtoto huyo anarudi huku analamba askrimu.

**JAMAA:** Maandazi yako wapi?

**MTOTO:** Wakati nafika yanapouzwa maandazi, nikagundua nimepoteza hela.

**JAMAA:** Halafu ikawaje?

**MTOTO:** Ila bahati nzuri wakati narudi ili kuja kukuambia kuhusu kupotea kwa hela yako, njiani nikaokota 1000 ambayo kuna mtu alipoteza ndio nikaamua kununua askrimu.

**JAMAA:** DUH

SWALI
Samaki nyangumi ana sifa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kipigo anachonipa mume wangu kimenichosha najipanga tuachane

MPENZI msomaji, tuendelee na uchambuzi wetu kuhusu masuala ya familia hasa eneo la ndoa. Yapo mambo ukiyasikia hadi unacheka.

Mfano hii tabia waliyo nayo wanaume wengi ya kupiga wake zao hata kwa jambo dogo linalohitaji kusameheana kisha maisha yasonge mbele. Mama akichelewa mahali kidogo tu ni kosa, anaambulia kichapo.

Yuko mama mmoja msomaji mzuri wa safu hii, alinipigia simu kunielezea mambo anayopitia katika ndoa yake iliyodumu kwa miaka sita sasa. Tayari wanandoa hawa wana watoto wawili.

Anasema, pamoja na ukweli kwamba alifurahia maisha ya ndoa mwaka wa kwanza na ule wa pili, ile mingine mine hadi sasa imekuwa ni mateso makubwa. Ni miaka ya misukosuko hakuna mfano wake.

Mama huyu aliwahi kuzozana na mumewe akampiga kipigo kilichoambatana na kumng'ata meno ya kutosha, hali iliyomfanya atoroke na mtoto mdogo na kumuachia mumewe yule mkubwa. Wakati huo alikuwa kwenye masomo ya chuo kikuu akisaka digrii yake.

Anasema: "Kisa cha kunipiga kilitokana na wivu. Hataki nipigiwe simu na wanachuo wenzangu wanaoniulizia pengine muda wa majadiliano kwa vikundi. Hawa amekuwa akiwaita eti ni mabwana zangu.

Ninapojitetea ananipiga. Tena akawa anadai mimi sina akili na hata hizo maksi ninazopata katika masomo yangu huwa napewa bure hazitokani na akili zangu. Jambo hili limekuwa linanishangaza sana.

"Ndani ya miaka hiyo sita, mwanamume huyu amenipiga mara tatu. Na katika moja ya matukio hayo, ndipo nilipoamua kuondoka na mwanangu mdogo kwani alining'ata sana. Kikao cha upatanisho ngazi ya familia kilifanyika lakini ilishindikana.

"Tulitawanyika kila mtu kivyake kwa miezi sita ndipo akili zikaturudi tukatafutana na kukubaliana turudiane tulee watoto ambao walikuwa hawaelewi kinachoendelea.

Kilikuwa kipindi kigumu sana kwa watoto na pia mimi nilitaabika sana kwani nilikuwa mwaka wa pili wamasomo ya digrii. Lakini Mungu ni mwema alinitia nguvu nikamaliza kwa ushindi na kujitwalia digrii yangu."

Mama huyu anaendelea kusema kwamba hata pale waliporudiana baada ya vikao vya usuluhishi wa famiia, bado mizozo haikuisha na tabia ya mwanamume huyu kupiga haikumwachia.

Alionywa sana kutompiga lakini ikawa kama ndiyo kwanza amechochewa moto. Wakati mwingine ilihitajika tu kuonyana na kusameheana lakini mume alikuwa haelewi hilo.

"Katika kunipiga, alitumia ngumi, mateke na kunichapa kwa mkanda wake anaovaa. Pia ana tabia ya kung'ata kama nilivyoeleza hapo awali na imenitokea mara mbili.

"Katika kipindi chote nilichoishi na mwanamume huyu, sijawahi kufurahia ndoa, ni mateso nakosa amani. Sasa imetosha najiandaa kufungua shauri la talaka mahakamani ili kila mmoja atafute amani kivyake. Sheria ndiyo itakayotuamulia kuhusu malezi ya watoto ambao bado ni wadogo."

Anamalizia kusimulia.

Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha ya kile anachopitia bibie huyu. Kituko hiki kinanikumbusha tabia ya baba mmoja aliyekuwa akimpiga mkewe kila mara hasa pale arudipo toka kwenye vilabu vya pombe.

Kumbe huko kilabuni bwana huyo alikuwa na mwanamke mchepuko wake. Na kila anapokuwa naye, akirudi nyumbani lazima ampige mkewe. Mke huyu alizaa naye mtoto mmoja.

Mwanamke kuona kichapo kinazidi, siku moja akaamua kutoroka na mwanawe na kumwacha jamaa peke yake. Naye akaona isiwe shida akamwita Yule mchepuko ili aje waishi wote. Naye akakubali. Katika kudadisi mchepuko akajua kuwa mke yule aliondoka kwa kuchoshwa na kipigo.

Kibao sasa kikageuka. Kila wawili hawa wanapotoka kwenye pombe, mwanamke huyu ndiye aliyekuwa akimpiga yule mwanamume. Sasa mwanamume naye kuona kipigo kinazidi, akaamua kuikimbia nyumba yake na kumwacha mchepuko wake huyo.

Naye kuona mwenzake harudi, akafungasha virago akarudi kwenye maskani yake.

Yule mwanamke aliyetoroka na mwanawe akapata mwanamume mwingine akaolewa sasa anaishi maisha ya amani, mwanawe anatunzwa na bwana huyo na tayari ameshamzalia watoto wawili. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Mungu anasema atawatesa wale wakutesao. Pia kwamba atawarudishia maadui zako ubaya wao.

Hakika kile unachowatendea wengine ndicho utakacholipwa wewe.Huna sababu ya kulipa kisasi kwa wabaya wako kwani kisasi ni cha Mungu mwenyewe. Pia ajidhaniaye amesimama, aangalie asianguke.

Niishie hapa. Je, una kisa ungependa tujadili? Nitumie ujumbe mfupi kupitia 0715 268581. Namba hii pia ipo WhatsAp. Tukutane wiki ijayo.

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Upatikanaji wa taarifa bado changamoto kubwa

KILA Septemba 28, ni siku ya haki ya upatikanaji wa taarifa ambayo iliasisiwa na wadau wa haki ya upatikanaji wa taarifa waliokutana nchini Afrika Kusini mwaka 2011 na kuja na tamko la Afrika lijulikanalo kama Jukwaa la Afrika la Upatikanaji wa Taarifa.

Lengo la tamko hilo lilikuwa kushinikiza; moja, mataifa ya Afrika kuwa na sheria za haki ya kupata taarifa, na pili, dunia kuasili Septemba 28 kama Siku ya Kimataifa ya Haki ya Kupata Taarifa.

Aidha, kampeni hiyo ilisababisha Umoja wa Mataifa kupitia la Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCOO la Novemba 17. 2015 kuitangaza rasmi Septemba 28 kuwa Siku ya Kimataifa ya Haki ya Kupata Taarifa, ambayo kwa nchini imechangia kwa kiasi kikubwa kupitishwa kwa Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa ya mwaka 2016.

Nchi mbalimbali duniani kote huadhimisha siku hiyo kwa namna tofauti. Kwa sisi Tanzania Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (MISA- TAN) iliadhimisha siku hiyo juzi kwa kutoa kufuli kwa taasisi au wizara iliyofungia taarifa na ufunguo kwa iliyofunguka zaidi.

Utafiti uliofanywa na MISA-TAN ulijumuisha taasisi nane za umma kati ya hizo kuna wizara nne na taasisi wakala wa serikali nne.

Kwa mwaka huu, taasisi zilizohusika katika utafiti huo ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Wizara ya Utalii, Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia , Wazee na Watoto.

Zingine ni Wizara ya Elimu, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL),

Aidha, mtafiti alipeleka barua za maombi ya taarifa zilitumwa kwenye taasisi hizo na zilitolewa siku 21 kupata majibu kama ilivyo katika sheria ya haki ya upatikanaji wa taarifa.

Tovuti za mashirika na taasisi hizi zilitafitiwa ili kuona ni aina gani ya taarifa za umma hutolewa na kwa namna gani.

Zaidi ya hayo. watafiti pia walitembelea ofisi hizo na kupiga simu kwa nyakati tofauti kama njia ya kujihakikishia upatikanaji wa taarifa mbalimbali kutoka kwa watumishi wa umma.

> **"Zingine ni Wizara ya Elimu, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL).**

Kwa kila njia iliyotumika alama zilitolewa kwa kila taasisi na hivyo kupata mshindi, mathalani kama taasisi ilijibu barua ndani ya siku 7 baada ya kupotea maombi, alama zake ni tofauti na walijibu siku 14 baadaye na ni tofauti na ambao hawakujibu kabisa hata baada ya siku 21 kupita.

Aidha, matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuna ofisi ambazo ukipiga simu saa kazi haiwezi kupokelewa, na wakati mwingine unaweza kudhani labda mhusika katoka kidogo. Lakini unapopiga simu mara kadhaa kwa nyakati na siku tofauti bila majibu, inatia shaka sana.

Pia, walibaini kuna mabadiliko makubwa katika matumizi ya tovuti kwa kuwa taasisi nyingi zimefanya vizuri katika eneo hilo lakini cha kushangaza pia ni kwamba, unaweza kupiga simu kuulizia taarifa fulani, ukaambiwa haipo ama wahusika hawana ruhusa kuitoa, lakini ukienda kwenye tovuti, unaikuta taarifa hiyo.

Aidha, matokeo yalibainisha kuwa WCF waliongoza kwa kutoa taarifa kwa umma kwa kuwa hata walivyopigiwa simu ilipokelewa, walijibu maswali na walimwalika mtafiti kupata taaria zaidi ofisini kwao, lakini zipo ambazo zilifanya kinyume chake.

Kwa mujibu wa utafiti TTCL ilipata kufuli kwa kufungia taarifa kwa kuwa njia zote zilizotumika kwenye utafiti hazikuwa na majibu.

Ifahamike kuwa njia zote zilizotumika ni ambazo mwananchi wa kawaida anaweza kuzitumia kutafuta taarifa, mathalani namba za simu zilizowekwa kwenye tovuti mbalimbali kutokupokelewa au kufanyakazi kabisa ni ishara kwamba bado kuna tatizo mahali.

Taarifa zinazotafutwa na wananchi ni zile za kisera na majukumu ya taasisi husika lakini ushirikiano ulikuwa mdogo, jambo linaloonyesha kuwa bado kuna kazi ya kufanya kuhakikisha wananchi wanapata taarifa kwa wakati.

Yako mambo mengi na mazuri yanafanywa na serikali kama ya miradi ya maendeleo ambayo umma unapaswa kuyajua, na ni wakati muafaka kutoa taarifa pale zinapohitajika.

## HARUSI









**Ilikuwa siku ya furaha kati ya Stephen Matoke na Stephanie Mzunguwanzala, walipofunga ndoa katika kanisa la Katoliki Parokia ya Roho Mtakatifu, Kitunda jijini Dar es Salaam. Ndoa ilifungwa Mei 2, 2020**



## MITINDO



Mbunifu wa mitindo, Aisha Kisoki. **PICHA: MITINDONITE**

# KIKOI

## Vazi la kale lisilochuja utamu

VAZI aina la Kikoi huko nyuma lilikuwa likivaliwa na wanaume, hasa katika ukanda wa Pwani.

Ukifika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Zanzibar ilikuwa ni kawaida kuwaona wanaume wakifanya shughuli zao huku wakiwa na vikoi kiunoni.

Hata hivyo, siku hizi vazi hili limekuwa likitumiwa na watu wa jinsia zote, huku kila wakati ikiibuka mitindo mipya kwa ajili ya kuwaridhisha wavaaji wake.

Wabunifu wa mitindo wanaendelea kutoa matoleo mapya ya vazi hilo, ikiwamo mashati, suaruali, kaptula, magauni na hata makoti yake.

Kwa jumla kuna aina nyingi ya vikoi, ikiwamo ile ya rangi nyeupe na mistari pembeni na vyenye rangi na muonekano wa batiki.

Wataalamu wa mitindo wanasema, nguo za vikoi huwa hazimtupi mtu na ni nzuri kutumia kama vazi la kwenda nayo ofisini, katika makongamano, burudani na hata michezo.

Kwa ujumla mvaaji anatakiwa kuhakikisha anachagua rangi nzuri inayolingana na ngozi yake pamoja na ubora wake.

Miguuni unaweza kutupia viatu va aina tofauti, kama vile viatu vya wazi, buti au viatu virefu.

URREMBO







NYWELE BANDIA

# Raha na karaha zake

MATUMIZI ya nywele bandia kwa wanawake ni jambo la kawaida, fedha nyingi zinatumika kwa ajili ya kupata urembo huo.

Nywele zipo za aina mbalimbali, lakini maarufu ni zile zinazosukiwa kichwani na zingine zinawekwa katika kofia maalum, maarufu kama wigi.

Uvaaji wa nywele za aina hii ni katika kujiweka katika muonekano wa kupendeza zaidi.

Lengo la utumiajai wa nywele hizi, ni kujiweka katika mtazamo mzuri na unaovutia machoni mwa watu.

Historia, inaonyesha nywele za bandia zilianza kutumia zamani na wanawake wenye asili ya Afrika wanaoishi Marekani, ambao walitumia kama njia ya kuepuka vitendo vya kibaguzi.

Hata hivyo, kila mabadiliko yalipotokea ndipo matumizi yake yalipozidi kuakisi na kuonekana kama moja ya pambo muhimu katika urembo.

**JE KUNA FAIDA?**

Faida zinazojulikana kwa mtumiaji wa nywele bandia ni pamoja na kubadilisha muonekano wake, kumpa mvuto na kumzidishia hadhi.

Wanawake wanaopenda nywele za aina hizi, mara nyingi wanaonekana wa kisasa na wenye kujiamini pale wanapokutana na wenzake.

**JE KUNA ATHARI?**

Baadhi ya wataalamu wa afya, wanasema nywele za bandia zina athari mbalimbali kama zikitumika kila mara.

Baadhi ya athari hizo ni kusababishia mzio kama malighafi au kemikali zilizotumika kutengeneza zitasisimua mfumo wa kinga ya mwili wa mvaaji.

Matatizo mengine ni kupata mba kutokana na kukosa hewa ya kutosha ya Oksijeni katika ngozi ya kichwa.

Aidha, unaweza kusababisha nywele kupata madhara na kunyonyoka endapo uchafu ukizidi.

Kwa wale wanaosukia kichwani wanapata maumivu ya kichwa.

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Kashata za nazi





**MAHITAJI**

SUKARI kikombe kimoja, nazi kikombe kimoja na mdalasini iliyosagwa nusu kijiko cha chai.

Maziwa vijiko viwili vya chakula na unga wa ngano kama utapendelea au rangi.

**NAMNA YA KUANDAA**

Pasua nazi, toa ile nyama ya ndani weka kwenye blender, weka na maziwa saga mpaka iwe laini sana. Au unaweza kukuna kwa kutumia kibao cha mbuzi.

Washa moto, bandika sufuria jikoni ikipata moto weka sukari, koroga mara kwa mara mpaka iyeyuke na kua rangi ya kahawia.

Punguza moto, weka nazi, mdalasini, rangi, unga koroga vizuri kwa dakika mbili mpaka mchanganyiko uwe mzito.

Chukua sinia ipake mafuta, toa mchanganyiko jikoni umwage kwenye sinia, chukua kijiko, usambaze uenee vizuri na uache upoe kwa muda.

Kata saizi unayotaka ukiwa bado wa moto, ukimaliza uache upoe kisha uanze kufurahia mlo wa kashata zako kwa chai, kahawa au kiburudisha kinywa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Pendezesha nyumba kwa gharama nafuu



BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha mwonekano.

Na mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa.

Leo tunakupa mwanga tu wa namna ya kuboresha maisha ya nyumbani kwako kwa gharama nafuu na ukabaki unafurahia maisha.

Matumizi tofauti ya rangi, karatasi za ukutani, vitambaa na malighafi nyingine zilizotengenezeza samani zako vina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa mwonekano wa nyumba yako na kukupa wa kuvutia zaidi.

Kwa mfano kupaka rangi upya kabati la runinga, miguu ya kiti au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa, kunasaidia kubadilisha mwonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili nakshi za mapambo kama pazia pamoja na fimbo zinazoshikilia pazia hizo, zuria, na mapambo ya ukutani. Vipo vitu ni vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke, kwa mfano kubadili rangi ya ukuta nayo ni mbinu nyingine.







Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo. Kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na wakati wa sasa.

Usiikatie tamaa nyumba yako kwa sababu inawezekana kuirudisha katika ubora wake.

Kikubwa ni ubunifu na kuongeza vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako, hata kama huna kipato kikubwa inawezekana, si lazima uweke vyote kwa wakati mmoja.

# Dondoo jinsi ya kuanika nguo zako ndani ya nyumba

**1:** Unaweza kununua chuma maalum kinachotumika kuanikia nguo ndani ya nyumba au tumia kamba zilizofungwa katika mbao.

**2:** Weka katika chumba ambacho hakina muingiliano wa watu ili zisichafuliwe.

**3:** Bana nguo zako na vibanio kuzuia zisianguke chini.

**4:** Hakikisha chumba kina hewa za kutosha ili nguo zikauke vizuri.






# KATUNI

## KATUNIKA KI'DOMOKRASIA

BY ABDUL KINGO - 2020

SMS - 0621 412 879












## JUKWAANI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...NG'OMBE HAKAMULIWI NA NJAA

HABARI KIMATAIFA



Rais Donald Trump, akiwasili katika viwanja vya hospitali ya jeshi la Taifa ya Walter Reed, iliyopo Bethesda, nchini Marekani juzi **(PICHA: AP)**

# Rais Donald Trump alazwa hospitalini

## ■ Ni baada ya kuambukizwa corona

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amekimbizwa katika hospitali moja ya kijeshi, siku mbili baada ya kuthibitishwa ameambukizwa virusi vya corona.

Taarifa iliyotolewa na Ikulu ya nchi hiyo, ilisema kiongozi huyo alipelekwa hoapitali ya Walter Reed baada ya kuwa na homa na uchovu.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilieleza hali yake si mbaya na alipelekwa huko kwa ajili ya matibabu kama hatua ya tahadhari.

Rais Trump, alichomwa sindano akiwa ndani ya Ikulu, baada ya mke wake Melania Trump, kugundulika kuambikizwa ugonjwa wa Covid-19.

Trump alipelekwa hospitali ndani ya saa 24 baada ya kuthibitishwa naye amepata virusi vya corona.

Imebaki mwezi mmoja pekee kabla ya kufanyika uchaguzi wa urais, Rais Trum anapigania kurudi madarakani kwa kumkabili mpinzani wake Joe Biden, kutoka chama cha Democratic. Akiwa amevaa barakoa na suti, rais huyo alitembea hatua ndogo kutoka ndani ya Ikulu ya White House, hadi alipopanda helikopta yake ambayo ilimpeleka hospitalini.

Katika kuonyesha yupo sawa, Trump aliwanyooshea mkono waandishi wa habari na kuweka ishara kuwa yuko sawa.

Katika mkanda wa video iliyowekwa kwenye mtandao wa Twitter, Rais Trump alisikika akisema "Nataka kumshukuru kila mmoja na mimi naenda hospitali ya Walter Reed. Nafikiri naendelea vizuri.

"Lakini tutahakikisha mambo yanakwenda sawa," alisema.

Aliendelea "Mke wangu pia anaendelea vizuri, asanteni sana, nawashukuru, siwezi kuwasahau asanteni."

**BBC**

# Armenia yaanzisha vita vikali

**YEREVAN, Armenia**

VIKOSI vya jeshi la Azerbaijan, vimeanzisha mashambulizi makali kwenye eneo la Nagorno-Karabakh, ambalo linagombaniwa na nchi jirani ya Armenia.

Taarifa zilizotolewa na Wizara ya Ulinzi ya Armenia, zilisema vikosi hivyo vimesonga mbele kutoka pande mbili za kusini na kaskazini ya jimbo hilo. Ilisema kulikuwa na mapigano makali kwenye eneo hilo linalodhibitiwa na raia wenye asili ya Armenia ambao wanataka kujitenga kutoka Azerbaijan.

Hata hivyo, imekuwa vigumu kuthibitisha taarifa hizo pamoja na zile zinazodai imezidungua ndege tatu za kivita za Azerbaijan.

Mataiafa yenye nguvu duniani, yametoa wito wa kusitishwa mapigano hayo.

Vyanzo kutoka Armenia vinasema hadi kufikia sasa mapigano hayo yamesababisha vifo vya watu 200, lakini upande wa Azerbaijan unasema ni watu 19 pekee wamekufa na wengine 60 wamejeruhiwa.

**DW**

# Sudan, waasi wakubaliana amani

**JUBA, Sudani Kusini**

SERIKALI ya Sudan na viongozi wa makundi ya waasi, jana walitarajia kutiliana saini mkataba wa amani unaolenga kumaliza vita vilivyodumu kwa muda mrefu.

Waziri Mkuu wa Sudan, Abdalla Hamdok, wakuu wa serikali ya mpito na viongozi wa vikundi yya waasi kutoka majimbo ya Darfur, Kordofan ya Kusini na Blue Nile walihudhuria katika tukio hilo la kihistoria.

Hafla ya kutiwa saini mkataba huo ilifanyika katika mji mkuu wa Sudan Kusini, wa Juba.

Pia wawakilishi kutoka Misri, Qatar na Saudi Arabia ni miongoni watu walioohudhuria.

Waziri Mkuu, Hamdok, alisema amani itafungua milango ya maendeleo na ustawi kwa watu Sudan.

**DW**

# Pakistan yazuia habari ya ubakaji

**KARACHI, Pakistan**

PAKISTANI imezuia vyombo vya habari kuripoti kisa cha kubakwa kwa mwanamke mmoja na kundi la watu mbele ya watoto wake.

Tukio hilo limetokea baada ya ofisa mmoja wa polisi kumlaumu mhanga wa mkasa huo.

Mamlaka inayosimamia vyombo vya habari nchini humo, iliamuru vituo vya televisheni na magazeti kuacha kuripoti taarifa hizo baada ya polisi kuonya inaweza kuvuruga ushahidi.

Shirika la kutetea haki za bindamu la Amnesty International na taasisi binfsi za kutetea haki za binadamu, waliomba kuondolewa kwa ofisa huyo wa polisi aliyemlaumu mwanamke aliyepatwa na mkasa huo kwa kutembea peke yake nyakati za usiku.

Tukio hilo lilitokea mwezi uliopita lilizusha maandamano ya wanaharakati wa haki za binadamu na watetezi wa wanawake .

Hadi sasa polisi ilimkamata mshukiwa mmoja, lakini ilishindwa kumtia nguvuni mshukiwa mkuu.

**DW**

MAKALA

# Uzee si laana



Na Magabilo Masambu

OKTOBA mosi ya kila mwaka, dunia huungana pamoja kuadhimisha siku ya wazee duniani. Siku hii ilianzishwa na Umoja wa Mataifa ikiwa na lengo la kuikumbusha jamii katika mambo kadhaa yanayowahusu wazee, haki zao msingi kama uhuru, ushiriki, huduma za kijamii, ulinzi, heshima, kulinda utu wao na mambo mengi yanayowahusu kama hayo.

Hapa Tanzania kwasasa tunaendelea na mchakato wa uchaguzi mkuu ambao unatarajiwa kufanyika Oktoba 28, 2020. Sote kwa pamoja nafikiri tunahitaji kusikia kutoka kwa wagombea ni kwa namna gani wazee watapewa kipaumbele katika huduma za kijamii na hasa eneo la afya (matibabu) ambalo ni tatizo kubwa zaidi pamoja na lishe bora.

Wapo watu imefika mahali wanadhani kuwa uzee ni laana kutokana na matatizo, mateso na manyanyaso wanayoyapata wazee wetu kwamba yanatokana na laana ya mambo waliyofanya wakiwa vijana.

Pengine jambo hilo lina ukweli fulani kwa baadhi yao kwamba hawakuwajibika vilivyo walipokuwa vijana au walitumia vibaya walichozalisha wakiwa vijana, lakini hii ina maana gani kwetu? Kwasababu hata tukiendelea kufikiri hivyo na tukaona njia sahihi ni kuwaacha waendelee kuteseka, sina hakika kama tutakuwa tumewafanya warudi ujanani ili waweze kujipanga tena, lakini hatuna namna ya kubadili yaliyopita, tunayo nafasi yakubadili yajayo.

Ni lazima tufahamu sote kwamba kama Mwenyezi Mungu akituhurumia tukaishi zaidi, basi uzee itakuwa ni njia ya kila mmoja wetu na hivyo hatuna budi kuweka mipango thabiti sasa ili tutakapozeeka basi uzee usionekane kama laana bali baraka za Muumba wetu.

Iko wapi thamani ya wazee sasa? Ni kweli kwamba jamii ya sasa inathamini uwepo wa wazee? Nafikiri tunapaswa kurudi tulikotoka, nakumbuka tukiwa wadogo tulipokuwa tukicheza mpira ilikuwa akipita mkubwa au mzee sote tulisimama na kuushika mpira apite kwanza, ili kuepusha kumpiga na mpira huo, au ilipotokea mzee akapita na mzigo na pengine hafahamu kwa mwenyeji wake tulimsaidia mzigo na kumpeleka mpaka anakokwenda kama ni jirani, yakowapi haya leo? Tunakwama wapi?

Taratibu tulianza kudharau umuhimu wa wazee jambo hili limeleta matatizo mengi sana kwenye jamii, hata kwenye eneo la uongozi vijana hawaoni tena cha kujifunza kwa wazee waliowatangulia katika nyadhifa zao, wanaona wanafahamu zaidi hawahitaji ushauri tena na kwamba ushauri wa wazee umepitwa na wakati, tumeenda mbali zaidi mpaka sasa kwenye familia hatuheshimiani tena, wote ndani ya familia tuna ndevu kama jamii ya kambare, nafikiri kwa kufanya hivi kuna vitu tunavikosa ambavyo vitatugharimu zaidi katika maisha yetu ya kila siku.

Bibi na babu zetu walitulea tukiwa wadogo hatujitambui hawakutunywesha sumu tufe, leo tumekuwa watu wazima tunatakiwa nasi tuwalee, tunasema sasa ni wachawi na kwamba wanapaswa kuuawa kwakuwa wana macho mekundu, lakini tumesahahu kwamba walitulea katika mazingira magumu, wakipikia kuni na kusababisha moshi kuathiri macho yao.

Wakati mwingine linaweza kuonekana jambo la kawaida sana unapokuwa na wazazi au wazee na umuhimu wao usionekane, lakini nakuhakikishia yatakuwa majonzi na majuto watakapotoka, wakati mwingine ukipitia magumu unasema angekuwepo mzee wangu, ningemshirikisha hili na lile kwahiyo Watanzania tusisubiri wazee wetu wafe ndiyo tuone umuhimu wao tuwajali angali wakiwa hai.

Tunayo makundi mawili ya wazee, moja ni wale waliokuwa na ajira rasmi za umma au binafsi, la pili ni wale wasiokuwa na ajira yoyote, makundi yote mawili wapo wenye watoto na wapo wasiokuwa na watoto katika dunia hii.

Ushauri wangu kwa serikali ijayo uwepo utaratibu wa pensheni ya wazee wote bila kujali kwamba aliajiriwa au la! Kumekuwapo na huduma zisizo na uhalisia mfano afya kwa wazee, ukweli ni kwamba wazee wanalipa sasa kwa asiye na pensheni wala hana mtoto wa kumtunza analipa vipi?

Tuwalinde, tuwaheshimu, tuwapende, tuwajali, tuombe ushauri kwao kwani wazee ni hazina nao wataiona thamani yao kwetu. Familia, jamii wala taifa halitapata laana ya wazee wetu hawa kinyume chake ni laana.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mabera na upinzani wa Msondo, Sikinde



Na Adam Fungamwango

LEO ni siku ya sita tangu mwanamuziki mkongwe nchini, Said Mabera, alipofariki dunia nyumbani kwake, Goba jijini Dar es Salaam na kuzikwa kesho yake jioni kwenye makaburi ya huko. Mabera aliyezaliwa mwaka 1949, alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 71.

Mabera aliyekuwa akiipigia bendi ya Msondo Ngoma Music, alijiunga na bendi hiyo mwaka 1973 akitokea National ya Arusha akiwa na Hassan Bitchuka, aliyekuwa pia kwenye bendi hiyo.

Historia inaonyesha kwamba Mabera tangu ajiunge na bendi hiyo, hajawahi kuihama hadi alipofariki dunia, akishikilia rekodi ya kuwa mmoja wa wanamuziki wachache duniani waliokaa kwenye bendi moja kwa muda mrefu zaidi.

Kingine ni kwamba tangu alipopata uongozi wa bendi mwaka 1977, aliendelea kuwa nao hadi alipofariki dunia usiku wa Septemba 28, mwaka huu. Hii ni kwamba amedumu Msondo Ngoma kwa miaka 47 na ameiongoza bendi hiyo kwa miaka 43.

Si tu kwamba mashabiki wa Msondo watamkumbuka kama kiongozi wa bendi, mpiga solo na mtunzi tu, bali kwa uongozi wake imara na shupavu, akiiongoza bendi kwenye nyakati zote za raha, amani na misukosuko ambayo bendi hiyo imepitia.

Wakati anajiunga, bendi hiyo ilikuwa inaitwa NUTA Jazz lakini wakati anapewa uongozi ilikuwa imeshabadilishwa jina na kuitwa Juwata Jazz na baadaye OTTU Jazz, kabla ya kuwa Msondo Ngoma Music Band.

Mabadiliko yote hayo yalitokana na jina la chama na shirikisho la wafanyakazi kubadilishwa kutoka NUTA, JUWATA, OTTU na hatimaye TFTU na TUCTA. Baada ya shirikisho la wafanyakazi kujitoa katika umiliki, wanamuziki na wadau wengine waliamua kuimiliki na kuwa Msondo Ngoma Music.

Kutokana na TFTU kujitoa katika umiliki, wanamuziki Mabera, TX Moshi William, Muhidini Gurumo, Athumani Momba waliamua kuisimamia na kukopa vyombo vya muziki kwa kuweka rehani amana zao na bendi ikaendelea kusonga mbele.

Mabera ataendelea kukumbukwa pale bendi ilipokuwa ikichukuliwa wanamuziki tegemeo na ilionekana kama inazidiwa nguvu au kwenda kufa kabisa. Lakini kwa uongozi wake imara na shupavu alisaka wanamuziki wengine ambao waliinua bendi.

Bendi iliyoonekana kutaka kuiua Msondo ni Mlimani Park Orchestra 'Sikinde Ngoma ya Ukae'. Ilikuwa ikimchukua kila mwanamuziki aliyeonekana anaing'arisha Msondo na kwao kuwa tishio. Na kwa sababu hiyo kukazuka upinzani mkubwa kati ya bendi hizo mbili hadi leo, ingawa kiasili Sikinde ilitakiwa iwe na upinzani na Dar International 'Super Bomboka' ya Majirani Rajab kwani Mlimani Park Orchestra iliundwa na wanamuziki karibu wote kutoka huko.

Msondo na Sikinde ni kama Simba na Yanga kwani zimejizolea mashabiki wengi nchini, ingawa baadhi hawajui upinzani huo ulitokana na nini. Upinzani wa Msondo na Sikinde ulianza mwaka 1979, mwaka mmoja baada ya Sikinde kuundwa.

Awali Msondo ilikuwa na upinzani na bendi za Dar Jazz na Western, lakini zilipokufa, mshindani halisi wa Msondo ilikuwa Urafiki Jazz.

Ilikuwa kama utani tu. Aliyekuwa kiongozi wa bendi ya Msondo na mpiga solo wake, Abel Balthazar alipoondoka kwenda kuunda Dar International mwaka 1977, ndipo Mabera alipoachiwa solo na kupewa uongozi pia.

Mwaka mmoja baadaye, karibu wanamuziki wote wa Dar International walijiengua na kwenda kuunda Mlimani Park Orchestra. Marijani ambaye awali alikuwa kwenye bendi hiyo, lakini akatimuliwa baadaye, aliitwa ili aifufue upya Super Bomboka.

Balthazar na wenzake walipokwenda kuunda Sikinde, waliwasomba pia wanamuziki kutoka Msondo wakiwamo Gurumo, Shaaban Dede, Suleiman Mwanyiro na Hassan Bitchuka. Hapo ndipo zilipoanza kuibuka nyimbo za mafumbo na vijembe kutoka bendi hizo ukiwamo wa Taraka Rejea wa Sikinde.

Pamoja na utani huo, Msondo chini ya Mabera ilikuwa ikisimama imara na kutoa vibao vilivyotikisa nchi, huku pia Sikinde ikifanya hivyo.

Miaka mingi baadaye kuanzia 1982 na 1985, Sikinde iliacha kufanya hivyo nayo ilipopata wababe wake, Bima Lee na Orchestra Safari Sound zilipokuwa zikigawana kutwaa wanamuziki wa bendi hiyo, hapo Msondo ikapumua.

Msondo na Sikinde ni bendi zilizojichukulia mashabiki wengi kutoka kila kona ya nchi. Mashabiki wa Sikinde ambao walikuwa wakienda dansini walikuwa wa kawaida, huku Msondo ikisifika kuwa na mashabiki wababe, watemi, wakorofi na watoto wa mjini.

Kwenye makala zijazo nitaelezea vituko vilivyokuwa vikifanywa na mashabiki wa bendi hizi kongwe pinzani ambazo mpaka sasa zipo na zinaendelea na upinzani, ingawa ule ubabe wa zamani kwa sasa hakuna tena. Ni ustaarabu kwenda mbele.


HADITHI

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Kati ya vijana hao, mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe kutokuwa na msimamo, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja-2

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**




AKIWA chumbani kwake juu ya kochi, Mashaka alikuwa akiwaza jinsi gani kilichotokea jana yake kule hospitalini.

Alihisi kama hakuwa yeye, ila ilikuwa ni ndoto mbaya sana aliyowahi kuota kwenye maisha yake.

Kila akiweka akili yake sawa, inamwambia kuwa lilikuwa tukio halisi na si ndoto.

hali kadhalilika, hakutegemea msichana kama Cecilia amdhalilishe vile. Kudhalilika ni jambo moja lakini kudhalilishwa na mtu ambaye umempa dhamana ya moyo wako ni jambo linalouma zaidi.

Udhalilike na mtesi wako, halafu uende kufarijiwa na mtu unayempenda ni jambo linalopendeza sana. Lakini si na mtu uliyetokea kumpenda.

Wakati mwingine akawaza kama yule ndiye Cecilia anayemfahamu au ni mtu mwingine aliyebadilishwa bila yeye kufahamu.

"Cecilia wa mwaka mmoja ulipota si huyu." alijiambia Mashaka.

"Bwana wee, ondoka na vichungwa vyako, kwani umesikia mama yangu ana upungufu wa damu?

"We Badaka, kuwa na heshima. Mimi dada yako ee, nani shemeji yako? Huyu kinyago?" Ni maneno ambayo bado yalikuwa yakijirudia kwenye ubongo wake.

Yalikuwa ni maneno ya kuudhi, kukera, kukasirisha na ya kukatisha tamaa kwa wakati mmoja yakitoka kwenye kinywa cha Cecilia yakielekezwa kwake pale kwenye nje ya Hospitali ya Mwananyamala.

Kwa mbali machozi yalianza kumtoka. Kila akifikiria alichomkosea mpenzi wake hakioni.

Mawazo yalirudi tena nyuma na kukumbuka alivyokutana na Cecilia.

Alikuwa akienda Chamazi kwa rafiki yake. Ndani ya daladala alikaa siti moja na mrembo mmoja hivi.

Mashaka alikuwa na gazeti la Nipashe la Wikiendi ambalo huandika na mambo ya burudani.

Kulikuwa na habari za wasanii wa bongo fleva, warembo na wacheza filamu. Wakati Mashaka akilipitia, aligundua kuwa msichana yule alivutiwa na habari za burudani kwani aligeuza kichwa na kuuangalia ukurasa huo kwa makini.

Akashindwa kufungua kurasa nyingine. Akampa gazeti lote. "Soma tu dada."

"Ahsante kaka." alisema Cecilia kwa sauti nyeyekevu, tamu masikioni na ya upole, huku akitabasamu.

> **"Mimi naitwa Mashaka. Naishi Ubungo Maziwa. Ni mfanyabiashara wa kawaida tu, ningependa hapa isiwe mwisho wa kufahamiana. Kila mmoja aende akakokwenda, lakini siku si nyingi tukutane tuyajenge, sawa Cecy?"**

Hakutaka kumsumbua dada wa watu. Alimwacha asome mpaka amalize kila alichotaka kukisoma.

"Ahsante sana kaka." Mashaka alisikia tena sauti ya dada huyo na alipogeuka, alikutana na mkono wa dada huyo ukiwa ameshika gazeti la Nipashe akilirudisha.

"Poa dada, ahsante na wewe."

Baada ya hapo, hakukuwa tena na ukuta baina yao. Badala ya ukuta kulijengwa daraja. Ikawa rahisi kwao kuwasiliana.

"Dada waenda wapi?"

"Mimi?" Alijibu mrembo huyo na haikueleweka kama ni swali au jibu.

Mashaka hakujua amwambie "Ndiyo wewe" au anyamaze kimya. Wakati anafikiria jibu likatoka.

"Naenda Mbagala Charambe kwa mama mdogo." Sasa lilijibu swali la kwanza.

"Huku unaishi wapi?"

"Kinondoni."

"Samahani, nani utaitwa?"

"Cecilia."

"Oooh, jina zuri."

"Ahsante."

Mashaka alimtazama kwa makini Cecilia, japo kiujanjaujanja kwa sababu hata yeye, pamoja na yote alikuwa na tabia ya aibu na hasa ikizingatiwa ilikuwa mara ya kwanza kukutana na msichana huyo.

"Mbona mimi hujaniuliza?"

Cecy aliangua kicheko na kuishia kusema "Sina cha kukuuliza." alijibu akiangalia chini kwa aibu.

Tayari basi lilikuwa limeshafika Mbagala Kuu. Waliteremka. Wakaongozana kama walikuwa wote tangu mwanzo wa safari.

"Mimi naitwa Mashaka. Naishi Ubungo Maziwa. Ni mfanyabiashara wa kawaida tu, ningependa hapa isiwe mwisho wa kufahamiana. Kila mmoja aende akakokwenda, lakini siku si nyingi tukutane tuyajenge, sawa Cecy?"

Ceci hakujibu, ila alitabasamu tu. Sura yake haikutaka kabisa kuangalia na Mashaka. Kwa Mashaka naye ilikuwa ni afadhali kwake. Naye asingeweza kabisa kukabiliana na sura ya msichana kama yule ikimwangalia.

Walizungumza hili na lile. Wakabadilishana namba za simu. Kila mmoja akawa na ya mwenzie. Kwa siku mbili mfululizo hawakupigiana simu. Si kwamba kila mmoja alimsahau mwenzake.

Ukweli ni kwamba baada ya kuachana. Mashaka akili yake ikahamia kabisa kwa msichana yule.

Aliona huenda ndiye akawa msichana sahihi aliyekuwa akimhitaji. Alikuwa na kila sifa za kuitwa msichana mrembo. Baadaye pia awe mke wa mtu.

Hakutaka kumpigia haraka haraka kwa sababu mbili. Kwanza, isije ikaonekana kama amekufa na kuoza zaidi. Pili hakutaka kuonekana ni mtu mwenye tabia mbaya ya kupendapenda wasichana. Siku moja tu kupata simu yake tayari unaanza kumsumbua.

Siku ya tatu alimpigia simu. Wakazungumza mengi na kuahidiana kukutana baada ya siku nne. Na kweli walikutana maeneo ya Magomeni Usalama.

Maongezi yalianza. Yaliishia kwa kuwa wapenzi.

Ni kawaida tu kwa mwanaume na mwanamke wanapokutana mara ya kwanza hadi kuwa wapenzi au mtu na mke.

Mwanaume anaweza kukutana na mwanamke akaitwa baba, baadaye mjomba, halafu shemeji, siku nyingine kaka, tena na shikamoo juu. Mwisho wa siku akaitwa mpenzi, 'baby', na majina yote ya mapenzi, inawezekana kabisa baadaye akawa mume.

Mwanamke naye ni hivyo hivyo, anaweza akaitwa mama mdogo, kesho shangazi, dada, mwishoni akawa ndiyo mpenzi, au mke.

Hivi ndivyo ilivyokuwa pia ni Mashaka na Cecilia. Mapenzi yakanoga. Wakapendana haswa. Kila mmoja alijua anapendwa na mwenzake. Pamoja na hayo walikuwa bado hawajatambulishana kwa wazazi. Walikuwa wanajiandaa kufanya hivyo.

Aliyekuwa anajua mapenzi hayo ni Badaka. Mdogo wa Cecy ambaye alikuwa akifuatana naye wakati mwingine kwenda kwa Mashaka. Ndugu wachache na majirani ya Mashaka pia walilijua penzi hilo.

"Sasa limekwenda wapi?" Alijiuliza. "Cecy mpenzi wangu umekula nini?" Machozi yalizidi kumtoka. Dakika chache baadaye usingizi ukampitia, kabla ya kuamshwa na mlio wa simu na alipoiangalia jina lilikuwa la Cecy.

INAENDELEA JUMAPILI

HABARI BURUDANI

# VERA SINDIKA TENA

## Atoka kimapenzi na Brown Mauzo



MREMBO anayewatingisha wasanii wa Afrika Mashariki, Vera Sidika, amemuibua mpenzi wake mpya baada ya kubwagana na mwanamuziki Otile Brown.

Sindika ambaye urembo wake unawatoa udenda wanaume, sasa yupo katika mapenzi mazito na msanii mwingine wa muziki Brown Mauzo.

Maisha ya Sindika yamezungukwa na matukio ya mapenzi pamoja na maisha ya kifahali ambayo kila siku amekuwa akiyaonyesha katika mitandao ya kijamii.

# Barakah amaliza bifu kibabe



MSANII wa Bongo Fleva, Barakah The Prince, amezidisha joto kati yake na msanii Ali Kiba, baada ya kusema mwanamuziki huyo na meneja wake Seven Mosha, hawana pesa za kumlipa.

Akipiga stori na EATV, Barakah amesema ameamua kusamehe, kusahau na kutofuatilia yaliyotokea japo anaamini waajiri wake hao wa zamani bado wana kinyongo.

"Naomba leo tufunge mjadala wa Alikiba na Seven Mosha, sina noma na mtu yeyote labda wao ndiyo wana noma na mimi, nimezika na nimefukia muda mrefu sana maana hawawezi kuwa na pesa ya kunilipa," amesema.



# Dully Sykes akumbukia enzi hizo

MWANAMUZIKI mkongwe, Dully Sykes, amekumbuka enzi alizoanza kuwa maarufu, akisema kipindi hicho msanii alikuwa akitengeneza jina lake kwa kazi na sio mitandao ya kijamii.

Akizungumza katika kipindi cha Planet Bongo kinachorushwa na East Africa Radio, Dully Sykes amesisitiza hakuna kitu kinachoweza kumpa mtu umaarufu tofauti na kuchapa kazi.

"Kuwa tajiri au masikini ni majaliwa ya Mungu, mimi nilipata umaarufu kabla ya Facebook, WhatsApp, Instagram na Twitter, kazi ndiyo inambeba kufikia mafanikio, hakuna mzembe anayefanikiwa hata ukitumia mitandao yote kama huna juhudi haina maana " amesema Dully Sykes.

HABARI MICHEZO

# Uefa sasa kuruhusu mashabiki uwanjani

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka barani Ulaya (Uefa), limetangaza kuwa mashabiki wanaweza kurudi viwanjani katika mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ruhusa maalumu ya serikali za eneo husika.

Hayo yamesemwa katika hafla ya utoaji tuzo za wachezaji, makocha bora zilizofanyika Alhamisi wiki hii.

Itakumbukwa mashabiki waliacha kuhudhuria katika viwanja vya michezo tangu Machi mwaka huu na hadi sasa hawajaruhusiwa, lakini Uefa kupitia Rais wake, Aleksander Caferin, anaamini uwezekano huo kwa sasa upo.

Kuanzia mitanange ya baada ya mapumziko ya mechi za timu za taifa mwezi huu, mashabiki watakaoruhusiwa kuingia viwanjani ni asilimia 30 ya uwezo wa uwanja, lakini mashabiki wa timu za ugenini hawataruhusiwa kuingia.

Licha ya ruhusa hiyo, bado kanuni za kujikinga na corona zitaendelea kama kukaa umbali wa angalau mita moja kutoka mtu hadi mwingine, kuvalia barakoa pamoja na kanuni nyingine kuzingatiwa.

Uamuzi ya Uefa yanakuja baada ya mtanange wa Super Cup kati ya Bayern Munich dhidi ya Sevilla ambalo mashabiki 15,000 walihudhuria kushuhudia kabumbu hiyo iliyopigwa Budapest Septemba 24, mwaka huu.

Akizungumzia kurudi kwa mashabiki, Rais huyo wa Uefa, alisema hiyo ni hatua ya awali kuelekea mashabiki kurejea, lakini afya za binadamu ni muhimu na kipaumbele cha kwanza kwao.





# ARTETA AMSIFU LENO

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema kipa wake namba moja, Bernd Leno alionyesha kiwango cha hali ya juu kwenye mchezo wa Kombe la Carabao wakati Arsenal wakishinda kwa mikwaju ya penalti dhidi ya Liverpool.

Mchezo huo wa raundi ya 16 uliopigwa Uwanja wa Anfield, dakika 90 zilikamilika bila kufungana na kusababisha kuingia kwenye changamoto ya mikwaju ya penalti ambapo Arsenal ilishinda kwa 5-4.

Ushindi huo unakuwa wa pili kwa Arsenal kuishinda Liverpool kwa penalti baada ya mwezi mmoja kupita kwani ilisepa na taji la Ngao ya Jamii kwa ushindi wa Penalti 5-4.

Arteta amesema kuwa wana makipa wawili wazuri na wanaofanya kazi kwa umakini ndani ya Uwanja jambo ambalo linampa matumaini ya kufanya vizuri hatua inayofuata ambayo ni robo fainali na atakutana na Manchester City.

"Tuna makipa wawili wazuri ndani ya kikosi, wote wawili wanafanya vizuri ni suala la kufanya uamuzi nani nahitaji aanze," alisema Arteta.

"Leno amekuwa akitimiza majukumu yake vizuri ana kazi ya kuendelea hapo zaidi.

"Nina imani kubwa kwamba Leno atakuwa na wakati mzuri zaidi kusaidia Arsenal kwa siku nyingi zinazokuja."

# Solskjaer bado ana imani kusajili wapya

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema Manchester United inajua mtazamo wake kuhusiana na suala la usajili wa wachezaji wapya ikiwa dirisha la usajili linafungwa Jumatatu ya Oktoba 5, mwaka huu.

Wakati wapinzani wa Man United kwenye Ligi Kuu England wanafanya usajili mkubwa na muhimu, United wamekamilisha uhamisho wa staa mmoja tu, kiungo wa Uholanzi Donny van de Beek ambaye ametua United kwa dau la pauni milioni 40.

Mtendaji Mkuu wa Man United, Ed Woodward amenukuliwa akisema mitanange ya kuchezwa bila uwapo wa mashabiki viwanjani kumeathiri klabu hiyo kiuchumi.

"Klabu bado inaendelea kufanyia kazi mapendekezo yangu," alisema Kocha Solskjaer juzi Ijumaa akinukuliwa na Sky Sport.

Borussia Dortmund wamekataa ofa mbalimbali za United za kuhitaji kumsajili winga wake Jordan Sancho mwenye umri wa miaka 20, ambaye ni chaguo namba moja kwenye dirisha hili kubwa la usajili. Beki wa Porto na Brazil, Alex Telles naye anatajwa kuhitajika na United. "Wanafahamu mtazamo wangu, dirisha la usajili bado liko wazi ingawa limebakiza siku chache, kama kuna kitu kitatokea au la utafahamu.

"Kuna namna mbalimbali za kuifanya timu iwe bora, nimekuwa nikijifunza namna nzuri ya kuwatumia wachezaji waliopo kupata ubora wao, siwezi kutegemea mchezaji ambaye bado sijamsajili.

Nina wachezaji wengi hivyo ushindani wa namba ni wa kutosha" alisema Solskjaer. "Tunahitaji matokeo chanya. Hii ndiyo njia pekee ya kufanya timu kuwa na morali".



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAPATA KUNDI MCHEKEA EUROPA LIGI

Inaonekana kuwa kinara kwenye kundi hilo kwani timu hizo hazijawahi kuvuka hatua...

**NYON,** Uswisi

ARSENAL inaonekana kupewa kundi mchekea kwenye Ligi ya Europa ambapo imepangwa Kundi B.

**Timu zilizopangwa na 'Washikabunduki' hao katika mashindano ya msimu huu wa 2020/21, ni pamoja na Dundalk, Rapid Vienna na Molde.**

Arsenal ndio inaonekana kuwa kinara kwenye kundi hilo ambapo timu hizo hazijawahi kuvuka hatua ya 16-bora na hivyo, wao wanapewa nafasi kubwa ya kupenya.

Arsenal wamefuzu makundi ya Ligi ya Europa baada ya kuifunga Chelsea kwenye mchezo wa fainali ya Kombe la FA Agosti, mwaka huu.

Tottenham Hotspur wameingia kwenye Kundi J pamoja na mabingwa wa Bulgaria, Ludogorets, LASK na Royal Antwerp. Leicester City watacheza dhidi ya Braga, AEK Athens na Zorya Luhansk, wakati Kundi H lina timu za AC Milan, Lille, Sparta Prague na Celtic huku Rangers wakiangukia Kundi D na Benfica, Standard Liege sambamba na Lech Poznan.

Kwa mujibu wa ratiba ya michuano hiyo itakayoanza mwezi huu, makundi matatu yatacheza siku moja Oktoba 22.

**MAKUNDI YAPO HIVI**

**Kundi A:** Roma, Young Boys, Cluj na CSKA Sofia

**Kundi B:** Arsenal, Rapid Vienna, Molde na Dundalk

**Kundi C:** Bayer Leverkusen, Slavia Prague, Hapoel Beer-Sheva na Nice

**Kundi D:** Benfica, Standard Liege, Rangers na Lech Poznan

**Kundi E:** PSV Eindhoven, PAOK, Granada na Omonoia

**Kundi F:** Napoli, Real Sociedad, AZ Alkmaar na Rijeka

**Kundi G:** Braga, Leicester, AEK Athens na Zorya Luhansk

**Kundi H:** Celtic, Sparta Prague, AC Milan na Lille

**Kundi I:** Villarreal, Qarabag, Maccabi Tel-Aviv na Sivasspor

**Kundi J:** Tottenham, Ludogorets, LASK na Royal Antwerp

**Kundi K:** CSKA Moscow, Dinamo Zagreb, Feyenoord na Wolfsberger

**Kundi L:** Gent, Red Star, Hoffenheim na Slovan Liberec

## ZISIKUPITE

### BAYERN KWA HUDSON-ODOI

BAYERN Munich ipo kwenye mazungumzo na Chelsea kuhusu kumchukua winga wa timu ya Taifa ya England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 19 kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Sport Bild, via Mail)***

### DEMBELE HAKIELEWEKI BARCA

WINGA wa Ufaransa, Ousmane Dembele, mwenye umri wa miaka 23, amebadilisha mwelekeo kuhusu kujiunga na Manchester United - lakini klabu yake ya Barcelona haijaondoa uwezekano wa uhamisho wake. ***(L'Equipe via Mirror)***

### POGBA AMUITA BEMBELE

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 27, amempigia simu mchezaji mwenzake wa Ufaransa, Ousmane Dembele kumshawishi ajiunge na miamba hao wa Old Trafford. (Mundo Deportivo - in ***Spanish)***

### AMCHANGANYA SOLSKJAER

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anajiandaa kumuuza winga wake, Daniel James mwenye umri wa miaka 22, ili kupata fedha za kumsajili nyota wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(ESPN)***

### LEEDS YAKOMAA NA JAMES

KLABU ya Leeds United imeonyesha nia ya kumsajili James kwa kuipa ofa Manchester United ya pauni milioni 25. ***(Football Insider)***

### CHELSEA YAMGOMEA ALONSO

CHELSEA imeiambia Inter Milan ingependa kuona mlinzi wa kushoto raia wa Hispania, Marcos Alonso, anaondoka kwa usajili wa kudumu baada ya miamba hao wa Serie A kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kwa mkopo. ***(Goal)***

### HODGSON AMKANA NELSON

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, amesema hajafanya mazungumzo yoyote na mshambuliaji wa Arsenal, Reiss Nelson mwenye umri wa miaka 20, licha ya kuhusishwa na usajili wake. ***(Mirror)***

### TORREIRA AWASILI MADRID

KIUNGO wa Arsenal, Lucas Torreira, mwenye umri wa miaka 24, amewasili nchini Hispania kwa ajili ya kufanyiwa vipimo vya afya tayari kujiunga na Atletico Madrid.

### SPURS YAMFUATA MILAN

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili mlinzi wa kati wa Inter Milan, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25 raia wa Slovakia. ***(Standard)***

### ARSENAL KUMTOA SALIBA

ARSENAL ipo tayari kumpeleka kwa mkopo mlinzi wake wa kati, William Saliba mwenye umri wa miaka 19, ambaye Rennes imeonyesha nia ya kumtaka. ***(Guardian)***

### INTER KUMSAJILI MATTEO

KLABUA ya Inter Milan, inakaribia kumsajili mlinzi wa pembeni wa Parma, Matteo Darmian mwenye umri wa miaka 30, kwa ada ya awali ya pauni milioni 1.81. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

## Kitimtim cha Netiboli Muungano Desemba

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Ligi ya Muungano mchezo wa Netiboli yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Novemba 28 hadi Desemba 7, mwaka huu jijini Tanga.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Tanzania (Chaneta), Judith Ilunda, alisema mashindano hayo yatashirikisha timu 12 kutoka Tanzania Bara na Visiwani.

"Maandalizi ya Ligi ya Muungano yanaendelea vizuri, wachezaji wote wanaendelea na mazoezi," alisema Ilunda.

Alizitaja baadhi ya timu zilizothibitisha kushiriki mpaka sasa kutoka Tanzania Bara kuwa ni Jeshi Stars, JKT Mweni na Jiji Tanga wakati Tanzania Visiwani ni KVZ, Mafunzo, JKU, Zimamoto pamoja na Uroa.

Aidha, aliomba wadau mbalimbali kujitokeza kuyaunga mkono mashindano hayo ili kuwawezesha kutimiza malengo waliyojiwekea baada ya kukaa kipindi kirefu bila kufanya mashindano kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Tunaomba wadau mbalimbali kujitokeza kutuunga mkono ili tutimize mpango tuliojiwekea kuelekea katika mashindano hayo," alisema.

## Gofu Kombe la Waitara Oktoba

**Na Shufaa Lyimo**

MICHUANO ya Majeshi ya Gofu kuwania Kombe la Waitara, inatarajiwa kufanyika Oktoba 30, mwaka huu katika Klabu ya Lugalo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Msemaji wa Klabu ya Gofu Lugalo, Seleman Semunyu, alisema mpaka sasa jumla ya washiriki 100 wamejiandikisha kushiriki mashindano hayo.

"Siku tulipotangaza mashindano watu walijiandikisha wengi mpaka muda huu kuna washiriki 100 ambao wamethibitisha kushiriki," alisema Semunyu.

Alisema anaamini washiriki wengi watajitokeza kushiriki mashindano hayo kutokana na idadi kubwa ya watu ambao tayari wameshajiandikisha huku bado wakiendelea kujiandikisha.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kwa ajili ya mashindano, tunasisitiza watu waendelee kuja kuchukua fomu za kushiriki," alisema.



# NIYONZIMA, AGREY FITI KUIVAA KAGERA SUGAR

**Na Saada Akida**

BENCHI la Ufundi la Azam FC, limeeleza kufurahishwa na kurejea kwa nyota wao wawili, Agrey Morris na Ally Niyonzima wakati huu wakitarajia kushuka dimbani leo kuivaa Kagera Sugar katika mechi yao ya raundi ya tano ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Uwanja wao wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam leo saa moja usiku.

**Niyonzima aliumia katika mechi dhidi ya Tanzania Prisons iliyopigwa Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga wakati Morris aliumia katika mchezo dhidi ya Coastal Union na kukosa mechi mbili za Ligi Kuu hadi sasa.**

Azam ambayo inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kushinda mechi zake zote nne za mwanzo, huku ikiwa haijaruhusu bao hata moja, leo itataka kuendeleza mbio zake za ushindi dhidi ya Kagera Sugar ambayo nayo imetoka kushinda mechi yake ya kwanza ilipoichapa KMC FC.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Vivier Bahati, alisema tayari wachezaji hao wako fiti na walikuwa katika mipango yao ya mechi yao ya leo dhidi ya Kagera Sugar.

Alisema wamefanya maandalizi mazuri kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu katika mechi hiyo ambayo wanaamini itakuwa na ushindani mkubwa.

"Kagera ni timu nzuri, tunawaheshimu, itakuwa mechi ya ushindani mkubwa, kwa sababu tunahitaji kutumia vizuri uwanja wetu wa nyumbani na wao wanahitaji matokeo mazuri," alisema Vivier.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wanaendeleza wimbi la ushindi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yao ya kupambana kubakiza pointi tatu nyumbani.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema wamejipanga vizuri kutafuta pointi muhimu katika mechi hiyo ya ugenini.

Alisema kikosi chake kipo vizuri na wamekuja kutafuta pointi muhimu kwa kila mechi ili kujiweka sawa katika msimamo wa ligi hiyo.

"Mechi yetu itakuwa na ushindani mkubwa, wenzetu watakuwa nyumbani na sisi tupo ugenini, lakini wote tunahitaji kupata pointi muhimu katika mechi hiyo," alisema Mecky.

TULIENI...




Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere na beki Gardel Michael (aliyevaa kofia), wakifurahia mjini Morogoro jana na mashabiki wa timu hiyo muda mchache kabla ya safari ya kwenda Dodoma kwa ajili ya mchezo wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara dhidi ya wenyeji, JKT Tanzania utakaopigwa Uwanja wa Jamhuri leo. **MPIGAPICHA WETU**

# *Chilunda amfuata Msuva Morocco*

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Tanzania, Shaaban Iddi Chilunda, anatarajiwa kusaini mkataba wa kujiunga na Mouloudia Oujda ya Ligi Kuu ya Morocco.

Uongozi wa Klabu ya Azam umesema wamefikia makubaliano ya kumuacha mchezaji wao huyo kwenda Mouloudia D'oujda kukamilisha taratibu za mwisho za kujiunga na miamba hiyo ya soka Morocco.

Endapo Chilunda afanikiwa kujiunga na klabu hiyo atakuwa mchezaji wa tatu wa Kitanzania katika Ligi Kuu ya Morocco baada ya beki wa kushoto, Nickson Kibabage na viungo Simon Msuva ambao wanachezea Difaa Hassan El Jadida na Maka Edward wa Moghreb Tetouan.

Msuva mwenye umri wa miaka 26, ndiye aliyefungua mlango wa Watanzania kwenda kucheza Ligi Kuu ya Morocco baada ya kujiunga na Difaa El Jadida mwaka 2017 akitokea Yanga ya Dar es Salaam, akifuatiwa na Kibabage kutoka Mtibwa Sugar mwaka jana na Maka aliyetokea Yanga pia mwaka jana.

Chilunda aliibukia katika timu ya vijana ya Azam FC mwaka 2012 kabla ya kucheza mechi yake ya kwanza timu ya wakubwa mwaka 2016 na Agosti 7, 2018 akajiunga na CD Tenerife ya Hispania inayoshiriki Segunda Division (Daraja la Kwanza) kwa mkataba wa miaka miwili.

Hata hivyo, mambo hayakumuendea vizuri huko, akatolewa kwa mkopo kwenda CD Izarra ya Segunda Division B (Daraja la Tatu) kabla ya kurejea Azam FC mwaka huu.

# Michezo



Jumapili Oktoba 4, 2020
Nipashe

Arsenal yapata kundi mchekea Europa Ligi UKURASA 22

## WANA JAMBO LAO...



Wachezaji wa Simba, kutoka kushoto ni beki wa kulia Shomari Kapombe, winga wa kulia Bernard Morrison pamoja na beki wa kati, Pascal Wawa, ambao leo watakuwa na 'jambo lao' (kusaka pointi tatu) katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma watakapoivaa JKT Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

## Uefa sasa kuruhusu mashabiki uwanjani

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka barani Ulaya (Uefa), limetangaza kuwa mashabiki wanaweza kurudi viwanjani katika...



HABARI UK. 21

## Solskjaer bado ana imani kusajili wapya

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema Manchester United inajua mtazamo wake kuhusiana na suala la usajili...



HABARI UK. 21

# Chama, Onyango vitani Kenya

## ●●● Simba yawapeleka Dodoma kwanza kumalizana na JKT Tanzania leo, Bwalya na Kahata nao...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa wa soka nchini, Simba, wakitua salama jijini Dodoma jana, tayari kwa mchezo wa raundi ya tano ya Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania, nyota wanne wa timu hiyo Joash Onyango, Francis Kahata, Clatous Chama na Rally Bwalya, watakuwa na vita nyingine nje ya klabu watakapokutana uso kwa uso wakizitumikia timu zao za taifa Oktoba 10, mwaka huu.

**Simba ambayo ililala mjini Morogoro usiku wa kuamkia jana kabla ya jana hiyo kutua jijini Dodoma, itashuka katika dimba la Jamhuri leo, kuivaa JKT Tanzania ikitoka kuvuna pointi tatu dhidi ya Gwambina FC, wakati wenyeji wao hao wenyewe wakitoka kuchezea kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Coastal Union ya Tanga.**

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema mechi hiyo haitakuwa nyepesi, lakini anaamini kikosi chake kinaweza kupambana na kupata matokeo chanya kutokana na ari ya kila mmoja kutaka kucheza.

"Haitakuwa mechi nyepesi kwa kuwa kila timu inahitaji ushindi, lakini tunachohitaji ni kupambana na kupata alama tatu ili kuendelea kujiweka katika nafasi nzuri ya kutetea ubingwa," alisema.

Baada ya mechi hiyo, Simba haitakuwa na mechi nyingine ya Ligi Kuu hadi Oktoba 18, mwaka huu itakaposhuka Uwanja wa Taifa kuvaana na watani zao, Yanga kwenye mechi ya raundi ya sita.

Hata hivyo, ratiba inayofuata kwa sasa ni wachezaji walioitwa timu zao za taifa kwenda kujiunga nazo, wakati huu ambao Simba imetoa nyota 11 ambao ni Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohammed Hussein 'Tshabalala', John Bocco, Mzamiru Yassin, Jonas Mkude, Hamisi Ndemla (wote wameitwa Taifa Stars), wakati Chama na Bwalya wenyewe wakiitwa timu ya Taifa ya Zambia 'Chipolopolo' huku Onyango na Kahata wakitwa timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars.

Na kuelekea mechi hizo za kimataifa zilizopo kwenye Kalenda ya Fifa, Kenya itacheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Zambia katika Uwanja wa Moi Kasarani jijini Nairobi Jumamosi ijayo, Oktoba 10 mechi ambayo Onyango na Kahata watakuwa na kibarua kigumu dhidi ya wachezaji wanaocheza nao klabu moja Chama na Bwalya.

Akizungumzia mchezo huo, Onyango, ameelezea furaha yake kucheza dhidi ya kiungo wanayecheza naye klabu moja, Chama.

Onyango ambaye licha ya kujiunga na Simba msimu huu amecheza mechi zote za Ligi Kuu Bara chini ya Kocha Sven, ameitwa katika kikosi cha Harambee Stars ikiwa ni mara ya kwanza kwake kuitumikia timu hiyo ya taifa akicheza klabu nje ya Kenya, kwani mara zote alikuwa akiitwa akitokea Gor Mahia ya nchini humo.

Hata hivyo, kitendo cha kuitwa kwenda kucheza dhidi ya Chama, kimemfurahisha Onyango ambaye anaeleza: "Naweza kusema nimefurahi sana kukutana na 'teammate' (mchezaji mwenzangu wa timu moja), ambaye atakuwa anaichezea Zambia na hiyo itakuwa mechi nzuri."

Onyango pia amesema ni jambo kubwa kwake kwa mara ya kwanza kuitwa katika kikosi cha Harambee Stars kinachonolewa na Francis Kimanzi akiwa kama mchezaji anayekipiga nje ya mipaka ya Kenya.

Kikosi hicho cha Kimazi, Harambee Stars, kitakuwa na kibarua kigumu kuibuka na ushindi dhidi ya vijana wa Mserbia Milutin Sredojevic 'Micho' anayeinoa Chipolopolo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042